UTT AMIS
Asset Management and Investor Services

## KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS

# TAARIFA YA MWAKA YA MFUKO WA UWEKEZAJI WA JIKIMU

Jikimu Income Scheme
LIVE WELL ...YOU DESERVE IT

## KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2025

Jikimu
Income Scheme
LIVE WELL ...YOU DESERVE IT

# YALIYOMO

1. Ratiba na Ajenda za Mkutano ........ ii
2. Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili ........ 1
3. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili ........ 13
4. Barua ya Mwenyekiti wa Bodi ........ 16
5. Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko wa Jikimu ........ 19
6. Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko ........ 21
7. Taarifa ya Hesabu za Mfuko ........ 24
8. Taarifa ya Meneja kuhusu Uwekezaji ........ 29
9. Jarida la Habari ........ 38

Jikimu Income Scheme
Live Well ...You Deserve It

**KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS
MKUTANO MKUU WA WAWEKEZAJI WA
MFUKO WA JIKIMU JUMAMOSI TAREHE 20 DISEMBA 2025
UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA
JULIUS NYERERE –DAR ES SALAAM**

# RATIBA NA AJENDA ZA MKUTANO

| MTIRIRIKO WA SHUGHULI | | | |
|---|---|---|---|
| **S/N** | **MUDA** | **SHUGHULI** | **WAHUSIKA** |
| 1. | 06.30 - 08.00 | Kuwasili kwa Wajumbe na Kujiorodhesha | Wajumbe/Utawala |
| 2. | 08.00 - 08.10 | Matangazo na Shughuli za Utawala | MC/Utawala |
| 3. | 08.10 - 08.15 | Kuthibitisha Akidi na Kufungua Mkutano | Mwenyekiti wa Bodi |
| 4. | 08.15 - 08.30 | Utambulisho (Wakurugenzi, Menejimenti na Watoa Huduma wa Mfuko) | Mkurugenzi Mtendaji |
| 5. | 08.30 - 08.40 | Kupitia Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili | Wote |
| 6. | 08.40 - 08.55 | Kupitia Taarifa za Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili | Mkurugenzi Mtendaji |
| 7. | 08.55 - 09.25 | Barua ya Mwenyekiti kwa Wawekezaji | Mwenyekiti wa Bodi |
| 8. | 09.25 - 09.40 | Kupokelewa kwa Taarifa ya Mwaka<br>1. Mwangalizi wa Mfuko<br>2. Mkaguzi wa Hesabu<br>3. Taarifa ya Hesabu | <br>CRdB<br>KpMg<br>Mkurugenzi wa Fedha na Mipango |
| 9. | 09.40 - 10.10 | Kupokea Taarifa ya Meneja Kuhusu Uwekezaji | Mkurugenzi wa Uwekezaji |
| 10. | 10.10 - 10.30 | Kipindi cha Maswali na Majibu | Bodi/Watendaji |
| 11. | 10.30 -10.45 | Kufunga Mkutano | Mwenyekiti wa Bodi |

# 2 Muhtasari wa Mkutano wa Kumi na Mbili (12) wa Mwaka

## WALIOHUDHURIA (Kiambatisho "A")

### BODI YA WAKURUGENZI

1. Prof. Faustin R. Kamuzora - Mwenyekiti wa Bodi
2. Dkt. Judika L. King'ori - Mjumbe wa Bodi
3. Bw. Paul A. Maganga - Mjumbe wa Bodi
4. Bw. David E. Mwankenja - Mjumbe wa Bodii
5. Bw. Simon M. Migangala - Mkurugenzi wa Bodi

### WAJUMBE WA KAMATI ZA BODI YA WAKURUGENZI

1. Dkt. F. Magambo - Mjumbe wa Kamati ya Bodi
2. Bw. Lameck Kakulu - Mjumbe wa Kamati ya Bodi

### WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

1. Bw. Daniel Olesumayan - Mjumbe wa Kamati ya Bodi
2. Bi. Neema J. Jones - Mjumbe wa Bodi

### MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS

1. Bw. I. Wahichinenda
2. Bi. J. Msofe
3. Bi. S. Mgaya
4. Bw. D. Balima
5. Bw. D. Mbaga
6. Bw. S. Bujiku
7. Bw. S. Kaniki
8. Bw. R. Mwanga
9. Bi. J. Swai
10. Bw. P. Ndunguru
11. Bi. V. Abuogo
12. Bw. F. Bwalya
13. Bw. B. John
14. Bi. J. Mlimbila
15. Bw. M. Balati
16. Bw. H. Mnongane
17. Bw. B. Liwali
18. Bw. C. Chanjarika
19. Bw. J. Joseph
20. Bi. R. Maruma
21. Bw. J. Masoud
22. Bw. B. Lukinga
23. Bw. A. Mushi
24. Bw. W. Ramadhan
25. Bi. J. Njovu
26. Bi. V. Maheri
27. Bi. D. Milenge
28. Bi. W. Malya
29. Bi. H. Lashkoni
30. Bw. A. Mabruk
31. Bw. A. Ambari
32. Bw. J. Nyambo
33. Bw. S. Ivambi
34. Bi. S. Kapufi
35. Bi. Y. Masanyoni
36. Bi. A. Laurent
37. Bi. E. Simon
38. Bw. M. Mchanjila
39. Bw. J. Mwangomola
40. Bi. M. Minja
41. Bw. C. Josiah
42. Bi. M. Mashiku
43. Bw. F. Lushinge
44. Bi. D. David
45. Bw. S. Khatib
46. Bi. P. Kasilati
47. Bw. F. Mzoo
48. Bi. V. Mashindano
49. Bi. A. Omari
50. Bw. A. Kandila
51. Bw. A. Felecian
52. Bi. L. Malimiru
53. Bi. J. Mteri
54. Bi. A. Alex
55. Bw. D. Makassy
56. Bw. Straton Rugaitika
57. Bi. A. Kijaji
58. Bw. N. Mlembah
59. Bw. C. Kilawe
60. Bw. O. Mafuru
61. Bi. A. Kalinga
62. Bi. P. Kunambi
63. Bi. J. Kilimba
64. Bi. H. Swalehe
65. Bi. E. Kahabi
66. Bw. B. Raphael
67. Bw. S. Mahumi
68. Bw. L. Temela
69. Bw. N. Muhoji
70. Bi. A. Mwinuka
71. Bi. C. Ngunda
72. Bw. H. Njau
73. Bi. F. Mwalisito
74. Bi. T. Mpiluka

## 1.0 AKIDI NA KUFUNGUA MKUTANO

Mwenyekiti alifungua mkutano saa 08:15 Mchana kwa kuwakaribisha wajumbe walioweza kuhudhuria Mkutano wa 12 wa Mfuko wa Jikimu. Hii ilikuwa ni baada ya wajumbe kupokea taarifa ya akidi, ambayo ilionesha kuwa Wajumbe wenye vipande waliohudhuria walikuwa 115 ambao majina yao yapo kwenye kumbukumbu hizi kama Kiambatisho "A". Mkurugenzi Mtendaji alitoa taarifa kwamba idadi ya Vipande vilivyoandikishwa vilikuwa 29,807,510.89 sawa na asilimia 20.13 ya jumla ya vipande vyote vya Mfuko kiasi cha vipande 148,107,218.285. Taarifa iliendelea kueleza kuwa idadi hiyo ya vipande vilivyowakilishwa inakidhi akidi inayohitajika kulingana na Waraka wa Makubaliano (Deed of Trust) ya asilimia 10 ya jumla ya vipande vyote vya Mfuko na hivyo Mkutano ungeweza kuanza.

## 2.0 DONDOO/AJENDA ZA MKUTANO

Wajumbe walikubaliana na dondoo/ajenda zifuatazo:

1. Taarifa ya Akidi na Kufungua Mkutano
2. Kuthibitisha Dondoo/Ajenda za Mkutano
3. Utambulisho

4. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Uliopita
5. Yatokanayo na Kumbukumbu za Mkutano Uliopita
6. Taarifa ya Mwenyekiti
7. Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko
8. Taarifa ya Mkaguzi wa Mfuko
9. Taarifa ya Hesabu za Mfuko
10. Taarifa ya Meneja wa Mfuko kuhusu Uwekezaji
11. Kipindi cha Maswali na Majibu
12. Kufunga Mkutano

## 3.0 UTAMBULISHO

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwatambulisha Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya UTT AMIS, Wajumbe wa kamati za Bodi na Wawakilishi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA). Aliendelea kuwatambulisha pia Wawakilishi wa Benki ya CRDB ambayo ni Mwangalizi wa Mfuko, Wawakilishi wa Kampuni ya KPMG inayotoa Huduma za Ukaguzi wa Hesabu za Mfuko pamoja na Mwakilishi kutoka ofisi ya Hazina ambayo inasimamia Taasisi za Serikali ikiwemo UTT AMIS. Mkurugenzi Mtendaji alimalizia kwa kuitambulisha Menejimenti ya UTT AMIS pamoja na wafanyakazi wote waliokuwepo mkutanoni kwa ujumla.

## 4.0 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO ULIOPITA

Baada ya kuzipitia Kumbukumbu za Mkutano wa kumi na moja kifungu kwa kifungu, wajumbe walizithibitisha na kuzipitisha Kumbukumbu za Mkutano wa kumi na moja (11) uliofanyika tarehe 20 Novemba 2023.

## 5.0 YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO ULIOPITA

5.1 Kuhusu ununuzi wa vipande kupitia simu kuboreshwa kuwa kama ununuzi kupitia Benki, ilielezwa kwamba limetekelezwa, ununuzi kwa simu umeboreshwa, vipande vinagawiwa ndani ya siku moja baada ya manunuzi.

## 6.0 TAARIFA YA MWENYEKITI

6.1 Mwenyekiti aliwasilisha taarifa ya Mfuko wa Jikimu kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2024. Aliwakaribisha wajumbe kwenye Mkutano Mkuu wa 12 wa Mwaka wa Wawekezaji wa Mfuko wa Jikimu.

6.2 Alianza kwa kumshukuru Mhe, Dkt, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua kuiongoza Bodi ya Wakurugenzi ya UTT AMIS. Pia aliwashukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt Natu Mwamba na Msajili wa Hazina, Ndugu Nehemiah Mchechu kwa kumpatia miongozo mara tu baada ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya UTT AMIS. Aliwashukuru pia wawekezaji kwa kuendelea kuwa na imani kubwa katika mfuko wa Jikimu.

6.3 Mwenyekiti wa Bodi aliendelea kutoa shukurani kwa kumshukuru Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Ndugu Casmir Sumba Kyuki, kwa uongozi imara na kazi nzuri ya kuiongoza taasisi ya UTT AMIS na kuifanya kuwa moja kati ya taasisi zinazoongoza katika Soko la Mitaji na Dhamana nchini Tanzania na ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, na pia kumtakia afya njema na heri katika majukumu yake mengine.

6.4 Aliwaeleza wawekezaji kuwa, kwa zaidi ya miaka 20 ya uwepo wa UTT AMIS, ni dhahiri kuwa fedha nyingi zimetengenezwa na kugawiwa kwa wawekezaji. Aliendelea kuwaeleza kwamba, uwekezaji huu tulivu (Passive Investment) huwafanya wawekezaji kutengeneza faida huku wakiwa wamelala au wakiendelea kutekeleza majukumu mengine ya kimaisha. Mwenyekiti alimnukuu mwekezaji maarufu aliyefanikiwa sana, Ndugu Warren Buffet, ambaye aliwahi kusema, *"kama hutakuwa na namna ya kupata fedha wakati umelala, utafanya kazi mpaka utakapofariki."*

6.5 Aidha, Mwenyekiti aliwaeleza wawekezaji kuwa, kutokana na jitihada kubwa iliyofanywa na Menejimenti na wafanyakazi wote na usimamizi imara wa Serikali, hakushangazwa sana pale UTT AMIS ilipotangazwa kuwa mshindi wa jumla kwa taasisi zinazoendeshwa kwa ufanisi bora nchini Tanzania. Hakika alijisikia mwenye furaha pale alipokabidhiwa tuzo kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan jijini Arusha, wakati wa mkutano wa Wenyeviti na Watendaji wakuu wa Taasisi za umma tarehe 28 Agosti, 2024.

6.6 Taarifa ya Mwenyekiti iliendelea kueleza kwamba katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024, utendaji wa Mfuko uliendelea kuwa mzuri. Faida kwa wawekezaji ilikuwa kubwa zaidi ya kigezo linganifu (Performance Benchmark) ikiwa ni wastani wa faida ya asilimia 13.7 ikilinganishwa na asilimia 13.6 ya mwaka ulioishia tarehe 30 June 2023. Faida iliyopatikana imeenda sambamba na maendeleo ya soko na ni kubwa kuliko kigezo linganifu cha asilimia 11.2. Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia Juni 2024, thamani ya mfuko iliongezeka kutoka shilingi bilioni 20.0 iliyofikiwa tarehe 30 Juni 2023 hadi Shilingi bilioni 26.8 tarehe 30 Juni, 2024. Mwenyekiti aliwaeleza wawekezaji kuwa, ongezeko hili la thamani ya Mfuko limetokana na faida nzuri inayopatikana, matumizi ya teknolojia katika kufanya miamala ya uwekezaji, kuongezeka kwa Imani na elimu

juu ya faida zinazopatikana kupitia Mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

6.7 Taarifa ya Mwenyekiti iliwajulisha wawekezaji kuwa pamoja na vihatarishi vitokanavyo na taharuki ya hali ya kisiasa na vita katika sehemu mbalimbali duniani, hali ya uchumi nchini Tanzania iliendelea kuimarika kwani ulikua kwa asilimia 5.1 kwa mwaka 2023 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.4 kwa mwaka 2024. Ukuaji huu wa uchumi ni mzuri zaidi ya wastani wa ukuaji katika nchi za ukanda wa Jangwa la Sahara na nchi za ukanda wa Ushirikiano wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambao ni asilimia 3.4 kwa mwaka 2023 na makadirio ya asilimia 3.8 kwa mwaka 2024, kama ilivyokadiriwa na Shirika la Fedha Duniani (IMF). Pia, kwa mujibu wa taarifa za Benki Kuu ya Tanzania, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.1 mwezi Juni 2024 ikilinganishwa na matarajio ya kiwango kisichozidi asilimia 5.0 na matarajio ya nchi za ukanda wa Afrika Mashariki cha asilimia 8.0. Kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita viwango vya riba katika soko havikubadilika sana na hivyo kuashiria utulivu wa soko kwa ujumla. Kwa upande mwingine, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani ilipungua kwa kiwango cha asilimia 12.8 sababu kubwa ikiwa ni kubadilika kwa sera za nchi ya Marekani na madhara yatokanayo na taharuki ya vita katika bara la Asia.

6.8 Kuhusu maendeleo ya Soko la Mitaji na Dhamana, ilielezwa kwamba maendeleo mazuri yameshuhudiwa katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Dhamana mpya zimeorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na bei ya hisa zilizoorodheshwa zimeongezeka kama inavyooneshwa na Fahirisi (Tanzania Share Index). Katika kipindi cha mwaka kilichoishia tarehe 30 Juni 2024, kumekuwa na ongezeko la Fahirisi la asilimia 9.3 ambapo iliongezeka toka 4,091.8 tarehe 30 Juni 2023 hadi 4,475.2 tarehe 30 Juni 2024. Ongezeko hilo ni zaidi ya lile la tarehe 30 Juni 2023 ambalo lilikuwa ni asilimia 4.1. Shukrani zilitolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Serikali kwa ujumla kwa kuendelea kusimamia na kuweka mazingira bora ya biashara nchini.

6.9 Wawekezaji walielezwa kupitia taarifa ya Mwenyekiti kuwa viashiria vya kiuchumi vinaonesha kwamba Kampuni ya uwekezaji ya UTT AMIS pamoja na Mifuko inayoisimamia imeendelea kufanya vizuri. Kwa upande wa thamani ya Mifuko imeongezeka kutoka Shilingi Trilioni 1.5354 tarehe 30 Juni, 2023 hadi kufikia Shilingi trilion 2.2382 tarehe 30 Juni, 2024. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 702.8, sawa na asilimia 45.7 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 538.9, sawa na asilimia 54.0 kwa mwaka uliotangulia. Ongezeko la ukubwa wa Mifuko umetokana na ongezeko la idadi ya Wawekezaji 79,519, sawa na asilimia 52.7 waliojiunga katika Mifuko kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na Wawekezaji 47,480, sawa na asilimia 24.0 waliojiunga mwaka wa fedha uliotangulia. Kama nilivyosema hapo awali kwamba mifuko yote imetoa faida nzuri kwa wawekezaji wake. Faida kwa mfuko wa Jikimu ilikuwa asilimia 13.7.

6.10 Mwenyekiti aliwaeleza Wawekezaji kwamba, katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kampuni ya UTT AMIS ulioshia Juni 2024, kumekuwa na mafanikio makubwa zaidi ya ilivyotarajiwa. Mwenyekiti alitolea mfano wa thamani ya mifuko iliyokadiriwa kukua kutoka Shilingi bilioni 290.7 tarehe 30 Juni 2019 mpaka Shilingi bilioni 485.9 kabla ya kurekebishwa na kuwa Shilingi Trilioni 1.0079 tarehe 30 Juni 2024. Hata hivyo, thamani halisi ya mifuko mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2024, ilikuwa ni Shilingi Trilioni 2.2 ambayo ni mara mbili ya kiwango kilichotarajiwa. Wawekezaji walielezwa kuwa, katika kipindi cha mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango mpya, UTT AMIS inatarajia kukamilisha uboreshaji wa mifumo kama msingi wa kukuza biashara yake. Taasisi pia itaendelea kufanyia kazi vipaumbele, ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma na kuibua bidhaa zingine kwa maslahi ya Wawekezaji. UTT AMIS itaendelea kuboresha huduma za uendeshaji kuwa za kisasa zaidi na kuhakikisha kuwa wawekezaji wanapata faida nzuri zaidi kadiri ya maendeleo

6.11 Aidha, Mwenyekiti aliwajulisha wawekezaji kuwa, katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024, Kampuni ya UTT AMIS iliendelea na awamu ya mwisho ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wake wa miaka mitano ulioishia mwezi wa Juni 2024. Pia UTT AMIS ilitayarisha Mpango Mkakati mpya wa miaka mitano ambao umejikita katika kuifanya UTT AMIS kuwa mshiriki mkubwa zaidi katika Soko la Mitaji na Dhamana nchini Tanzania na ukanda wa Afrika Mashariki. Ili kuendana na kipindi cha mipango cha Serikali, Mpango Mkakati Mpya utafanyiwa mapitio ndani ya mwaka 2024/2025 ili uweze kumalizika mwezi Juni 2030. Mwenyekiti alisema, kati ya malengo yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati mpya ni pamoja na kukuza thamani ya mifuko kutoka Shilingi Trilioni 2.238 za sasa hadi Shilingi Trilioni 7.5 ifikapo Juni 2030 na kuongeza idadi ya matawi ili kusogeza huduma kwa wawekezaji nchini na nchi za Afrika Mashariki pamoja na nchi za ukanda wa SADC. Zaidi ya hapo,

Mpango Mkakati unaonesha kuwa huduma kwa wawekezaji zitakuwa za kidijitali. Katika kujiandaa na utekelezaji wa Mpango Mkakati mpya, UTT AMIS ndani ya mwaka huu wa fedha 2024/2025 imeanza na uboreshaji wa mifumo ili kuimarisha uwezo wa kumudu kiwango kikubwa cha biashara. Mradi huu wa kuboresha mifumo unatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili.

6.12 Hali kadhalika, Mwenyekiti aliwajulisha wawekezaji kuwa katika mkutano wa Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi uliyofanyika jijini Arusha, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyaelekeza mashirika ya umma ambayo yana uwezo, kuendesha shughuli zake za kiuchumi na zenye kuleta faida nje ya Tanzania. UTT AMIS ikiwa katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wake, inatarajia kuwafikia na kuwahudumia Wawekezaji wengi zaidi nchini Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na Ukanda wa nchi za SADC. Katika kutekeleza hilo, UTT AMIS imekuwa ikifuatilia maendeleo ya soko katika jumuiya hizo mbili kwa kipindi cha miaka kadhaa. Matokeo ya awali yanaonyesha kwamba baadhi ya nchi zina fursa nzuri. UTT AMIS itaimarisha na kuelekeza nguvu katika kuchambua masoko haya mapya ili kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati muafaka. Ukizingatia lengo la Mkakati la kuongeza thamani ya Mifuko, ni muhimu kuwa kila fursa inayopatikana iweze kutumika vyema. Kwa kuzingatia kuwa ninyi Wawekezaji mnazifahamu faida za uwekezaji katika mifuko inayoanzishwa na kusimamiwa na UTT AMIS, Mwenyekiti aliwaomba Wawekezaji waendelee kuwa mabalozi wazuri juu ya uwekezaji kwa familia, marafiki, ndugu pamoja na jamaa zao.

6.13 Katika kuhitimisha taarifa yake, Mwenyekiti aliwashukuru wote kwa ushirikiano na imani yao kwa UTT AMIS na Mfuko wa Jikimu kwa kipindi chote cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Kwa namna ya kipekee aliishukuru Serikali kupitia Wizara ya Fedha, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Mwangalizi wa Mifuko ambaye ni Benki ya CRDB, Soko la Hisa la Dar es Salaam pamoja na Madalali wake, Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, Wafanyakazi wa UTT AMIS na Wadau wote ambao wameendelea kuiwezesha UTT AMIS kutekeleza majukumu yake katika mwaka huu wa fedha. Alieleza matumaini yake kuwa ushirikiano huu utaendelea kwa manufaa ya Wawekezaji na maendeleo ya Soko la Mitaji na Sekta ya Fedha hapa nchini.

## 7.0 TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO

7.1 Mwakilishi wa Benki ya CRDB ambaye ni Mwangalizi wa Mfuko wa Jikimu, aliwasilisha Taarifa iliyoeleza kwamba, kama waangalizi wa Mfuko wa Jikimu, wana jukukumu la kusimamia na kuhakikisha kwamba utendaji wa meneja wa mfuko unaendana/ unazingatia waraka wa makubaliano ili kuhakikisha maslahi bora ya wenye vipande. Katika utekelezaji wa kazi hiyo, mwangalizi wa mfuko ana majukumu yafuatayo; Uangalizi wa mali za mfuko, kuhakikisha meneja wa mfuko anatumia njia/mbinu sahihi katika kukokotoa mahesabu ya thamani ya mfuko sambamba na mkataba wa makubaliano, na pia kuhakikisha viwango vya uwekezaji vinazingatiwa.

7.2 Mwakilishi huyo alieleza kuwa Katika kipindi cha mwaka wa fedha, kilichoanzia tarehe 01.07.2023 mpaka 30.06.2024, Benki ya CRDB kama mwangalizi wa mfuko wa Jikimu, imeendeleza uangalizi wa mwenendo wa shughuli za meneja wa mfuko, utekelezaji wake na kuangalia changamoto kwenye uwekezaji.

7.3 Mwakilishi wa Benki ya CRDB alihitimisha kwa kuwathibitishia Wawekezaji wa Mfuko kwamba shughuli za uwekezaji kwenye mfuko wa Jikimu na wajibu wa meneja wa mfuko (UTT AMIS), vimeendeshwa/ vimetekelezwa kufuatana na vipengele vya waraka wa makubaliano. Tukizingatia suala la imani/ uaminifu wa wenye vipande kwenye mfuko, tunathibitisha kwamba maslahi ya wenye vipande ndani ya mfuko wa Jikimu yanalindwa na kuzingatiwa ipasavyo, na meneja ameendesha mfuko kulingana na waraka wa makubaliano.

## 8.0 TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MFUKO WA JIKIMU

8.1 Mwakilishi kutoka Shirika la Wahasibu la KPMG ambao ni Wakaguzi wa Mfuko aliwasilisha Muhtasari wa Taarifa kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Mfuko kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024. Alieleza kuwa Taarifa ya Hesabu za Mfuko zilizowasilishwa yaani Taarifa ya Mapato na Matumizi, Taarifa ya Urari wa Hesabu za Mfuko, Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko na Taarifa ya Mtiririko wa Fedha umetayarishwa kutoka katika taarifa kamili ya ukaguzi ya Mfuko wa Jikimu kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024.

8.2 Taarifa ilieleza kuwa Muhtasari wa taarifa ya hesabu za fedha haioneshi taarifa zote kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha (International Financial Reporting Standards (IFRS)). Taarifa ya wakaguzi iliendelea

kusema Muhtasari huu wa hesabu pamoja na hii taarifa yetu siyo mbadala wa taarifa kamili ya hesabu za kifedha iliyokaguliwa. Muhtasari wa hesabu za kifedha pamoja na taarifa kamili ya hesabu zilizokaguliwa haijumuishi matukio au miamala baada ya tarehe za taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa.

8.3 Pia taarifa ilieleza kwamba maoni ya ukaguzi (Audit opinion) yasiyokuwa na kasoro juu ya taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha za Mfuko yalitolewa kwenye taarifa ya tarehe 11 November, 2023 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024. Taarifa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 inajumuisha mambo mengine muhimu juu ya ukaguzi wa hesabu za Mfuko.

8.4 Mwakilishi huyo alihitimisha taarifa yake kwa kueleza kuwa majukumu yao kama wakaguzi wa hesabu za Mfuko ni kutoa maoni kama muhtasari wa hesabu za Mfuko unaendana na taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha na kwa mujibu wa taratibu zao za ukaguzi, ukaguzi ambao ulifanywa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi (International Standards on Auditing–ISA) 810 (kama ilivyorekebishwa), kuhusu "Kazi za kuripoti juu ya Muhtasari wa taarifa za fedha".

## 9.0 TAARIFA YA MWAKA KUHUSU HESABU ZA MFUKO WA JIKIMU

Mkurugenzi wa Fedha na Mipango wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwasilisha Taarifa ya Hesabu za Mfuko kwa kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024.

9.1 Mkurugenzi aliwaomba wawekezaji kusoma taarifa kwa kulinganisha hali ya utendaji wa Mfuko kwa miaka miwili (2) iliyoishia mwezi Juni, 2024 na Juni 2023 na kwamba taarifa imegawanyika katika sehemu kuu nne, ambazo ni Taarifa ya Mapato na Matumizi (Statement of Profit or Loss and Other Comprehensive Income), Taarifa ya Urari wa Hesabu za Mfuko (Statement of Financial Position), Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko (Statement of Changes in Net Assets Attributable to Unit Holders) na Taarifa ya Mtiririko wa Fedha (Statement of Cash Flows).

9.2 Kwa upande wa Mapato na Matumizi, Taarifa ilieleza kuwa, katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024, jumla ya Mapato ya Mfuko yalikuwa Shilingi 3,986,048,000/= ikilinganishwa na Mapato ya Shilingi 3,018,406,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Kuongezeka kwa mapato kunatokana na kuongezeka kwa viwango vya faida ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji na mabadiliko ya soko. Pia ilielezwa kuwa jumla ya Gharama za Uendeshaji kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 zilikuwa Shilingi 644,702,000/= ikilinganishwa na Shilingi 497,016,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023, hivyo kufanya Faida baada ya kutoa gharama za uendeshaji na kabla ya kodi kuwa Shilingi 3,341,346,000/= ikilinganishwa na Faida ya Shilingi 2,521,390,000/=mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Mfuko ulilipa gawio kwa wawekezaji wake kiasi cha shilingi 1,668,561,000 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024 ikilinganishwa na shilingi 1,432,862,000 kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023, Kodi iliyotozwa na Serikali ilikuwa Shilingi 26,483,000/= ikilinganishwa na Shilingi 14,746,000/= kwa mwaka wa fedha 2023. Hivyo, Mfuko ulibaki na Faida Halisi (baada ya Kodi na Matumizi) ya Shilingi 1,646,302,000/= ikilinganishwa na Shilingi 1,073,782,000/= mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

9.3 Kwa upande wa Urari wa Hesabu za Mfuko, ilielezwa kuwa, Rasilimali za Mfuko zilikuwa ni Shilingi 27,155,015,000/= arehe 30 Juni, 2024, ikilinganishwa na Shilingi 20,130,751,000/= tarehe 30 Juni, 2023. Dhima za Mfuko zilikuwa na jumla ya Shilingi 951,776,000/= tarehe 30 Juni, 2024, ikilinganishwa na Shilingi 787,678,000/= tarehe 30 Juni, 2023. Kutokana na taarifa hiyo, thamani halisi ya Mfuko tarehe 30 Juni, 2024 ilikuwa ni Shilingi 26,203,239,000/= ikilinganishwa na Shilingi 19,343,073,000/= tarehe 30 Juni 2023.

9.4 Kwa upande wa Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko, thamani ya Mfuko Mwanzoni mwa Mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2024 ilikuwa Shillingi 19,343,073,000/= ikilinganishwa na Shillingi 17,882,664,000/= mwanzoni mwa Mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023. Ongezeko kutokana na faida ya Mfuko kwa kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2024 ilikuwa ni Shilingi 1,646,302,000/= ikilinganishwa na Shilingi 1,073,782,000/= kwa mwaka linganishi ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Kwa upande wa miamala ya wenye vipande, mfuko ulipokea (Net sales) kiasi cha Shillingi 5,213,864,000/= kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2024 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 386,627,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Miamala hiyo imepelekea mabadiliko ya thamani halisi ya Mfuko kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024, kuwa Shilingi 26,203,239,000/= ikilinganishwa na Shilingi 19,343,073,000/= kwa mwaka 2023.

9.5 Kwa upande wa Taarifa ya Mtiririko wa Fedha, ilielezwa kuwa fedha halisi iliyotokana na shughuli za uendeshaji kabla ya marekebisho ya mtaji kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024,

ilikuwa Shilingi 369,984,000/= ikilinganishwa na Shilingi 96,914,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Fedha halisi iliyopatikana kutoka kwenye shughuli za Uendeshaji baada ya marekebisho ya mtaji na kodi ya Serikali ilikuwa Shilingi 575,954,000/= ikilinganishwa na Shilingi 1,331,206,000/= kwa mwaka wa fedha 2023. Miamala ya Amana kwa wawekezaji ilipokelewa fedha kiasi cha shilingi 4,248,398,000/= tarehe 30 Juni, 2024 ikilinganishwa na malipo ya fedha kiasi cha shilingi 865,002,000/= tarehe 30 Juni, 2023. Miamala hiyo ilipelekea kubaki na salio la fedha kiasi cha Shillingi 4,824,352,000/= Mwaka wa fedha ulioshia 30 Juni, 2024 ukilinganisha na Shillingi 466,204,000/= 30 Juni, 2023. Aidha Mfuko ulikuwa na akiba ya Fedha kiasi cha Shilingi 704,313,000/= mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2024 ikilinganishwa na Akiba ya Shilingi 238,109,000/= mwanzoni mwa Mwaka wa Fedha 2023, Mfuko umeweza kubaki na Akiba ya fedha taslimu kiasi cha Shilingi 5,528,665,000/=, mwishoni mwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 ikilinganishwa na Shilingi 704,313,000/=, mwishoni mwa mwaka wa fedha wa 2023.

## 10.0 TAARIFA YA MENEJA WA MFUKO KUHUSU UWEKEZAJI

Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwasilisha Taarifa ya Meneja kuhusu uwekezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024.

10.1 Taarifa ilieleza kuwa kwa muda wa mwaka mmoja mfuko wa Jikimu umelipa gawio la shilingi 12.0 kwa kila kipande. Thamani ya kipande iliongezeka kwa shilingi 22.7 hadi kufikia shilingi 176.8 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi 21.4 kwa mwaka 2023. Ukubwa wa mfuko uliongezeka kwa shilingi bilioni 6.8 hadi kufikia shilingi bilioni 26.8 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 1.5 mwaka uliopita 2023. Faida ya Mfuko wa Jikimu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 ilikuwa asilimia 13.7 ikilinganishwa na asilimia 13.6. ya mwaka uliopita.

10.2 Taarifa iliendelea kueleza kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24, UTT AMIS kama meneja wa Mfuko alitumia uzoefu na weledi alionao katika kuhakikisha mfuko unafikia mgawanyo anuai wa rasilimali kwenye uwekezaji wake wenye kuleta tija huku akizingatia sera na miongozo mbalimbali inayotumiwa kwenye uwekezaji. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 mgawanyo anuai wa rasilimali za mfuko wa Jikimu umewekeza kiasi cha asilimia 23.4 kwenye hisa, kiasi cha asilimia 57.6 kwenye dhamana za serikali za muda mrefu na asilimia 19.0 kwenye amana za benki za muda mfupi. Mfuko uliwekeza zaidi kwenye dhamana za serikali za muda mrefu ili kujipatia mapato ya uhakika kwa muda mrefu. Aidha, uwekezaji katika amana za benki za muda mfupi (call account) umefanywa ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji wa mfuko ikiwemo kulipa fedha kwa wawekezaji pindi wanapouza vipande vyao.

10.3 Mwasilishaji alieleza mambo mengine muhimu ya kuzingatia wakati wa kulinganisha faida za uwekezaji katika Mfuko wa Jikimu pamoja na amana za benki; alieleza kuwa, viwango vya faida vinavyooneshwa ni kabla ya kutoa kodi ya zuio ya asalimia 10.0 (withholding tax) wakati faida ya mfuko wa Jikimu ni baada ya kutoa kodi ya zuio ya asalimia 10.0. Mfuko wa Jikimu unaruhusu wawekezaji kuuza vipande wakati wowote hivyo kumpa fursa ya kupata fedha pindi anapozihitaji (hulipwa ndani ya siku kumi (10) za kazi) na kwamba hakuna kiwango cha chini cha uwekezaji kisichopata faida. Viwango vya faida kwenye Mfuko vinatolewa sawa kwa wawekezaji wote (wawekezaji wa kipato kidogo, kipato cha kati na wale wenye kipato kikubwa). Aina nyingine za uwekezaji katika soko la fedha zina muda maalumu na ukomo, uwekezaji katika mfuko wa Jikimu hauna muda maalumu au ukomo.

10.4 Kuhusu pato la Taifa, meneja aliripoti kuwa kwa mwaka 2023 uchumi ulikua kwa kiwango cha asilimia 5.1, ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 4.7 mwaka 2022 (kama ilivyooneshwa kwenye jedwali III). Aidha, ilielezwa kuwa sababu zilizochagiza ukuaji wa Uchumi ni pamoja na kuwepo kwa hali nzuri kwenye shughuli za madini, kilimo na ujenzi vilikuwa vichocheo vikubwa vya ukuaji wa uchumi katika kipindi hicho. Hata hivyo, ukuaji wa uchumi mwaka 2023 ulionesha kuwa nchi ilitekeleza sera madhubuti na ilihimili madhara yatokanayo na vita zinazoendelea ulimwenguni. Hivyo, kwa mwaka 2024 kiwango cha ukuaji wa uchumi kinakadiriwa kukua kwa asilimia 5.4. Mwasilishaji aliendelea kueleza kuwa, hali hii ya mwenendo wa uchumi ni muhimu kwa mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS kwani inaonesha matarajio mazuri ya faida kwa wawekezaji.

10.5 Hali ya mfumuko wa bei nchini hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024 ilikuwa ni asilimia 3.1 ikilinganishwa na asilimia 3.6 iliyonakiliwa tarehe 30 Juni 2023. Aidha, ilielezwa kuwa viwango hivyo ni stahimilivu na vipo chini ya asilimia 5.0 ya kigezo linganifu kinachotumika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya maendeleo kusini mwa Afrika (SADC). Mwasilishaji alisema, mwenendo huu wa mfumuko wa bei umetokana na kuwepo kwa hali nzuri kwenye shughuli za kilimo na sera madhubuti. Aidha, mamlaka inakadiria hali ya

mfumuko wa bei kwa kipindi cha miaka mitatu hadi mitano ijayo kubaki chini ya asilimia 5.0. Kuwepo kwa hali nzuri ya mwenendo wa mfumuko wa bei nchini kumewezesha wawekezaji kuendelea kuwekeza kwa wingi. Hata hivyo, UTT AMIS inajitahidi kuwekeza kwenye maeneo yanayotoa faida zaidi ya kiwango cha mfumuko wa bei.

10.6 Kuhusu Sekta ya benki, meneja alieleza kuwa katika mwaka wa fedha ulioisha tarehe 30 Juni 2024, sekta ya benki ambayo inajumuisha sehemu kubwa zaidi ya sekta ya huduma ya fedha ilibaki imara, thabiti na yenye faida, ikiwa na mtaji na ukwasi wa kutosha. Jumla ya rasilimali ziliongezeka kwa shilingi trilioni 8.3 kutoka shilingi trilioni 53.7 iliyonakiliwa Juni 2023 hadi shilingi trilioni 62.0 Juni 2024. Kiasi cha amana za wateja kiliongezeka kwa asilimia 13.7 kutoka shilingi trilioni 35.7 hadi shilingi trilioni 40.6 Juni 2024. Pia mikopo kwa wateja ilifikia shilingi trilioni 37.4 ikilinganishwa na shilingi trilioni 31.5 mwaka uliopita. Mifumo ya malipo kwa njia ya kidigitali nchini iliendelea kuwa imara, ikithibitishwa na kuwepo kwa kiwango cha juu cha miamala iliyokamilika kwa muda mfupi. Kuwepo kwa mifumo imara na thabiti kumehamasisha umma kuendelea kuamini na kutumia mifumo ya kidigitali kwenye huduma mbalimbali za kifedha. Aidha, kwa mwaka 2023 idadi ya miamala iliyofanyika kutoka kwenye huduma za pesa mtandao kwenda benki ni milioni 6.6 yenye thamani ya shilingi trilioni 2.7. Kwa kipindi hicho, idadi ya miamala iliongezeka kwa asilimia 34.1 na asilimia 25.2 kwenye thamani. Aidha, Kuendelea kuimarika kwa sekta ya benki nchini ni muhimu kwa mifuko na wawekezaji kwa ujumla, kwani hali hio husaidia kuchochea shughuli za uchumi na huwarahisishia Wawekezaji kuwekeza kwenye mifuko ya UTT AMIS kwa urahisi zaidi. Wawekezaji walielezwa kuwa meneja wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja kwa sasa amefanikiwa kuunganisha mifumo ya UTT AMIS na benki ili kuwawezesha wawekezaji kununua vipande kwa njia ya kidigitali popote walipo.

10.7 Mwasilishaji aliwaeleza Wawekezaji kuwa, katika sekta ya mawasiliano idadi ya laini za simu za mkononi na mezani zilizosajiliwa imeongezeka kwa milioni 11.5 hadi kufikia milioni 75.5 mnamo Juni 2024 ikilinganishwa na ongezeko la laini milioni 7.8 mwaka uliopita. Aidha, idadi ya laini hizo za simu zilizosajiliwa ni zile zilizotumika angalau mara moja katika miezi mitatu iliyopita. Usajili wa akaunti za huduma za pesa mtandao (idadi ya akaunti) umeongezeka kwa asilimia 18.0 kutoka milioni 47.2 hadi milioni 55.7 mnamo Juni 2024. Jumla ya mauzo ya vipande yaliyopokelewa na UTT AMIS kupitia mitandao ya simu za mkononi ni shilingi bilioni 47.4 mwaka ulioshia tarehe 30 Juni 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 25.4 yaliyopokelewa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Halikadhalika, Mwasilishaji alieleza kuwa, kwa kipindi chote ukuaji wa sekta ya mawasiliano nchini umeleta matokeo chanya kwa taasisi ya UTT AMIS kwani umechochea na kurahisisha uwekezaji katika mifuko na kuboresha zaidi huduma binafsi. Kwa sasa kupitia simu za mkononi wawekezaji wanaweza kufungua akaunti, kuuza vipande, kuangalia salio na miamala waliofanya kwa kupiga *150*82# au kutumia programu tumizi (UTT AMIS APP) pamoja na kununua vipande kupitia huduma ya pesa mtandao. Pia, Wawekezaji walitaarifiwa kuwa UTT AMIS inatarajia kuongeza kiwango cha kutoa fedha kwenye uwekezaji (kuuza vipande) kwa siku kutoka kiwango kinachotumika sasa cha shilingi milioni 2 hadi milioni 5 kupitia simu za mkononi na UTT AMIS APP.

10.8 Kuhusu Dhamana za Serikali ilielezwa kuwa, kwa kipindi cha mwaka wa fedha ulioisha Juni 2024, uwekezaji kwenye dhamana za serikali katika soko la awali ulifanyika kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na mwaka uliopita. Kiasi cha dhamana za serikali za muda mfupi kilichouzwa kilipungua kwa shilingi trilioni 0.6 kutoka shilingi trillioni 3.3 hadi shilingi trilioni 2.7. Hata hivyo, uhitaji wa dhamana za serikali za muda mfupi uliongezeka kwa shilingi trilioni 0.7 hadi kufikia shilingi trilioni 4.3 kutoka shilingi trilioni 3.6 mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Kiasi kilichokubaliwa baada ya mnada kimeongezeka kwa shilingi trilioni 0.1 kutoka shilingi trilioni 2.5 hadi shilingi trilioni 2.6 Juni 2024. Katika soko la dhamana za serikali za muda mrefu, jumla ya shilingi trilioni 3.3 ziliuzwa ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.3 mwaka uliopita. Kiasi cha ushiriki kwa kipindi hicho kiliongezeka kwa shilingi trilioni 0.6 hadi shilingi trilioni 5.2 ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.6 mwaka uliotangulia. Kiwango kilichokubaliwa kilipungua kwa shilingi trilioni 1.1 hadi shilingi trilioni 2.8 kutoka shilingi trilioni 3.9 mwaka 2023. Aidha, Kuongezeka kwa ushiriki na uwekezaji kwenye dhamana za serikali kunaashiria ongezeko la uelewa kwa umma kuhusu uwekezaji na akiba. Hivyo, ongezeko la uelewa na ushiriki katika soko la dhamana nchini husaidia kuboresha ukwasi na faida kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

10.9 Kuhusu viwango vya Riba katika dhamana za serikali za muda mfupi Wawekezaji walielezwa kuwa, kwa mwaka wa ulioishia tarehe 30 Juni 2024, viwango vya riba vilivyotozwa kwenye amana za benki hazikubadilika kwa kiwango kikubwa. Ilielezwa kuwa, Wastani wa riba za mikopo ulikuwa asilimia 15.4 na riba kwa mkopo wa mwaka mmoja ni asilimia 15.8. Wastani wa

faida kwa amana za benki ni asilimia 7.5 na faida kwa amana ya mwaka mmoja ni asilimia 8.7. Aidha, Kiwango cha wastani wa faida kwenye dhamana za serikali za muda mfupi kiliongezeka hadi asilimia 8.3 mnamo Juni 2024 kutoka asilimia 6.5 mnamo Juni 2023. Kiwango cha riba kwa mikopo ya siku kwa benki kilipanda hadi asilimia 7.2 kutoka asilimia 5.0. Mwezi Januari 2024, kamati ya sera ya fedha (MPC) ya Benki Kuu ilianza kutumia sera mpya ya fedha kwa kutumia mfumo wa riba ya Benki Kuu (CBR). Riba hiyo iliongezwa hadi asilimia 6.0 mwezi Aprili 2024 kutoka asilimia 5.5 mwezi Januari 2024. Hata hivyo, ongezeko la faida kwenye uwekezaji wa dhamana hizo huleta matokeo chanya kwenye faida kwa wawekezaji.

10.10 Mwasilishaji alieleza kuwa, mnamo tarehe 30 Juni 2024, akiba ya fedha za kigeni ilifikia zaidi ya dola bilioni 5.0. Dola moja ya Marekani iliuzwa kwa shilingi 2,640.0 Juni 2024 ikilinganishwa na shilingi 2,339.1 mnamo Juni 2023, kwa kipindi cha mwaka mmoja shilingi ya Tanzania ilishuka thamani kwa asilimia 12.8 ikilinganishwa na asilimia 1.0 mwaka uliopita. Hata hivyo, Benki kuu ilichukua hatua kadhaa ikiwemo kuzuia utumiaji wa dola kwa mahitaji ya huduma na bidhaa zinazopatikana nchini. Hatua hizi zinatarajiwa kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni, kuongeza akiba ya fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya fedha ya Tanzania.

10.11 Kuhusu Soko la Mitaji na Dhamana, taarifa ilieleza kuwa kufikia tarehe 30 Juni 2024, ushiriki na uwekezaji kwenye soko la mitaji, dhamana na kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja uliongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita 2023. Kwa kipindi hicho cha mwaka mmoja, benki mbili za biashara na shirika moja la serikali ziliorodhesha hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 482.4 kama ifuatavyo; Hatifungani ya Kijani ya muda wa miaka 5 kwa faida ya asilimia 10.25 ya benki ya CRDB, hatifungani ya maendeleo na ya kijamii ya miaka 3 kwa faida ya asilimia 9.5 ya benki ya NMB, pamoja na hatifungani ya Mamlaka ya Maji Tanga kwa muda wa miaka 10 kwa faida ya asilimia 13.5 kwa mwaka. Aidha, mifuko miwili ya uwekezaji wa pamoja iliongezeka sokoni, kwani meneja aitwae Alpha Capital Ltd alizindua mfuko wa Alpha Halal na Zan Securities Ltd alizindua mfuko wa Timiza. Hali ya ushiriki kwenye soko la mitaji, dhamana na uwekezaji kwenye mifuko ya pamoja nchini imeongezeka, ni matarajio yetu kuwa hali hii itazidi kuimarika na kuongezeka zaidi. Kuingia kwa wasimamizi wapya wa mifuko (meneja wa mifuko) ya uwekezaji wa pamoja na fursa zingine za uwekezaji sokoni ni ishara nzuri kwa UTT AMIS na soko kwa ujumla, na tunatarajia taasisi au kampuni zingine kujiunga ili kuongeza ukwasi na ushindani jambo ambalo litaongeza zaidi ufanisi, faida na huduma bora kwa Wawekezaji.

10.12 Taarifa ya Soko la Upili kwa Dhamana na Hatifungani zilizoorodheshwa ilionyesha kuwa katika soko la upili, jumla ya thamani ya miamala ya dhamana za serikali za muda mrefu iliongezeka kwa shilingi trilioni 0.6 hadi kufikia shilingi trilioni 3.5 kutoka shilingi trilioni 2.9 mwaka uliopita. Thamani ya miamala ya hatifungani za kampuni binafsi zilizoorodheshwa ilikuwa shilingi bilioni 3.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.0 mwaka jana. Aidha, thamani ya miamala ya hatifungani za kampuni binafsi zilizoorodheshwa mwaka huu ni kubwa zaidi kwa shilingi bilioni 2.9 ikilinganishwa na mwaka jana. Ilielezwa kuwa, ongezeko la thamani ya miamala limetokana na kuongezeka kwa hatifungani mpya zilizoorodheshwa sokoni.

10.13 Kuhusu Soko la Hisa taarifa ilionyesha kuwa, mnamo tarehe 30 Juni 2024, thamani ya soko la Hisa la Dar es Salaam ni shillingi trilioni 16.8, ikiwa juu kwa asilimia 12.0 kutoka shillingi trilioni 15.0 mwaka jana. Asilimia ya ushiriki kwa wawekezaji wa ndani ni wastani wa asilimia 76.2, ikilinganishwa na asilimia 69.6 mwaka 2023. Pia, Fahirisi ya Hisa kwa kampuni za ndani (TSI), iliongezeka kwa asilimia 9.3 hadi kufikia alama 4,475.2. Fahirisi ya kampuni zote sokoni (DSEI) iliongezeka kwa asilimia 12.0 hadi kufikia 2,016.9. Jumla ya mauzo ya soko katika kipindi hicho, iliongezeka kwa shilingi bilioni 165.0 hadi shilingi bilioni 272.6 kutoka shilingi bilioni 107.6 mwaka uliopita. Katika kipindi hicho, baadhi ya kampuni zilitangaza na kulipa gawio kwa wanahisa. Gawio lililolipwa kwa kila hisa lilikuwa kama ifuatavyo; TCC - Sigara (Tsh. 500.0), TWIGA (TPCC) (Tsh. 390.0), TBL (Tsh. 537.0), NMB (Tsh. 361.18), SWISS (Tsh. 51.33), VODA (Tsh. 9.95), DSE (Tsh. 145.0) na CRDB (Tsh. 50.0).

10.14 Taarifa ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ilionyesha kuwa, kwa kipindi cha mwaka mmoja kilichoishia tarehe 30 Juni 2024, idadi ya washiriki na rasilimali imeongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita. Aidha, jumla ya rasilimali zinazosimamiwa sokoni ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 1,550.7 hadi kufikia shilingi bilioni 2,273.6. Soko limetambulisha mifuko mipya miwili ambayo ni Alpha Halal na mfuko wa Timiza. Aidha, Mwasilishaji aliwaeleza Wawekezaji kuwa rasilimali za mifuko na huduma za uwekezaji zinazosimamiwa na UTT AMIS zimeongezeka kwa shilingi bilioni 702.8 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 538.9 lililonakiliwa mwaka jana. Mabadiliko chanya katika jumla ya rasilimali yalionesha kuongezeka kwa imani ya wawekezaji katika bidhaa za UTT AMIS kutokana

na usalama, faida shindani na urahisi wa kuingia na kutoka kwenye uwekezaji.

10.15 Mwasilishaji wa taarifa alimalizia kwa kuwahakikishia Wawekezaji kuwa UTT AMIS itaendelea kubuni na kuvumbua mianya na fursa za uwekezaji kadiri inavyojitokeza katika soko ili kuongeza mapato na faida kwa Wawekezaji. Lengo likiwa ni kuvuka matarajio ya Wawekezaji kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

## 11.0 MASWALI, MAONI NA MAJIBU

### 11.1 Maswali na Maoni toka kwa Wawekezaji: -

111.1.1Pongezi nyingi zilitolewa kwa Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa UTT AMIS kwa kusimamia mifuko vizuri na kwa weledi wa hali ya juu na kuhakikisha faida inapatikana vizuri, hususani malipo ya gawio ambayo hulipwa kwa mpango wa kila robo mwaka.

11.1.2 Mwekezaji mmoja alitaka kupata ufafanuzi kuhusu usalama wa fedha za wawekezaji.

11.1.3 Mwekezaji aliomba ufafanuzi kuhusu ukubwa wa kodi kwa mwaka ulioishia Juni 2024 ukilinganisha na mwaka uliopita (2023).

11.1.4 Mwekezaji aliuliza ni kwa nini gawio limeshuka kutoka shilingi nne (4) hadi shilingi tatu (3) na je inawezekana kurudi kwenye shilingi nne kwa sasa?

### 11:2 Wawakilishi wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS walitoa ufafanuzi na Majibu ya maswali kama ifuatavyo:

11.2.1 Pongezi zilipokelewa na Meneja wa mfuko na kuahidi kuendelea kusimamia vizuri kwa weledi na maarifa ili kuwaletea faida shindani katika uwekezaji wao.

11.2.2 Kuhusiana na usalama wa fedha za wawekezaji, mwakilishi wa UTT AMIS aliwatoa wasiwasi wawekezaji juu ya usalama wa fedha zao na kuwaeleza kuwa UTT AMIS ni Taasisi ya Serikali na hivyo Serikali inalo jukumu la kulinda mali za wawekezaji. UTT AMIS inasimamiwa na CMSA ambaye jukumu lake ni kusimamia uendeshwaji wa masoko ya mitaji na dhamana na kufuatilia kuona kama waraka wa makubaliano unafuatwa na pia UTT AMIS ina mwangalizi wa Mifuko ambaye ni benki ya CRDB ambayo iko chini ya Benki Kuu (BOT) ambaye ni msimamizi katika tasnia ya fedha na Mkaguzi mkuu wa Serikali (CAG) na kampuni binafsi ya ukaguzi ya KPMG ambao huhakikisha fedha za wawekezaji ziko salama siku zote.

11.2.3 Ilielezwa kuwa, kwa suala la kodi inategemea zaidi na wapi fedha zimewekezwa, kwa mwaka unaoishia Tarehe 30 Juni, 2024 UTT AMIS iliwekeza zaidi kwenye sehemu zenye kodi ya zuio la asilimia 10 kama ilivyokuwa kwa mwaka uliopita 2023.

11.2.4 Kuhusiana na gawio kushuka hadi shilingi tatu kwa robo mwaka kutoka shilingi nne, ilielezwa kuwa, kipindi gawio linatolewa kwa shilingi nne, soko lilifanya vizuri kwa miaka hiyo na kulingana na soko lilivyo kwa wakati huu UTT AMIS imezingatia kutoathiri mitaji ya wawekezaji hivyo iliona ni vizuri kutoa kiasi hicho cha shilingi tatu kwa robo mwaka huku mitaji ya wawekezaji ikiendelea kukua.

## 12. KUFUNGA MKUTANO

Baada ya kutamatika kwa kipindi cha maswali na Majibu, Mwenyekiti aliwashukuru Wawekezaji wote kwa kuhudhuria katika Mkutano huo. Pia aliwahakikishia kuwa mawazo na mapendekezo yaliyotolewa katika Mkutano huu yatazingatiwa na yale yanayowezekana yatatekelezwa. Mwisho aliwatakia heri ya sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya 2025. Mkutano ulifungwa saa kumi na dakika arobaini na tano (10:45) jioni.

................................... ...................................

**MWENYEKITI** **KATIBU**

...................................

**TAREHE**

Ikimu Income Scheme
LIVE WELL ...YOU DESERVE IT

# KIAMBATISHO "A"

## ORODHA YA WAWEKEZAJI WA MFUKO WA JIKIMU WALIOHUDHURIA KWENYE MKUTANO WA KUMI NA MBILI (12) WA MWAKA WA MFUKO ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KITUO CHA KIMATAIFA CHA JULIUS NYERERE, DAR ES SALAAM TAREHE 20 NOVEMBA 2024

| S/NO. | JINA LA MUWEKEZAJI |
|---|---|
| 1. | ABEdNEgO MESHACK MOLLEL |
| 2. | AdAM EdWARd MARANdU |
| 3. | AgNES THOBIAS MKAMATI |
| 4. | AINEA YOSIA KATONdO |
| 5. | ALEX CHIpANdA SENEdA |
| 6. | ALEX CHIpANdA SENEdA |
| 7. | ALISTId SAMBA HIgINI |
| 8. | AMIRI dAMAS MSHANA |
| 9. | AMON BONIpHACE KARAMBA |
| 10. | ANESI SATOKI MAHENgE |
| 11. | ANgELA pETER MApUNdA |
| 12. | ANNA JONASAI MApHOLE |
| 13. | ANTHONY ABRAHAM MKWESO |
| 14. | ASHRAF ABdALLAH gONZA |
| 15. | AURELIA IgNAS KApINgA |
| 16. | AYUBU LAZARO SIZYA |
| 17. | BARAKA RASHId MAdENI |
| 18. | BEATRICE pARMENAS KISIMBO |
| 19. | CARLTON JUSTIS LYARUU |
| 20. | CHARLES KASHASHA MUTALEMWA |
| 21. | CHRISTINA LUCAS MATERU |
| 22. | CHRISTINE pATRICIA MATAKA |
| 23. | COTWU (ZANZIBAR) |
| 24. | dAVId RWEgOSHORA MUKELA |
| 25. | dISMAS RApHAEL NTABINdI |
| 26. | dOMINIC pETER gANdYE |
| 27. | dOREEN KOMBA |
| 28. | ELIA SILVESTER MLELEU |
| 29. | ELIREHEMA WILSON URIO |
| 30. | ELIZABETH dOSLA gEAY |
| 31. | EMILIAN pASCHALIS BUSARA |
| 32. | EMMANUEL THOMAS MFUKO |
| 33. | EMMANUEL YUSUpH CHUWA |
| 34. | ERASTO BAYNETH CHIWANgA |
| 35. | EZEKIA ANdREW MHIMBA |
| 36. | FATIMA SIMON KIONgOSYA |
| 37. | FLORA LINUS OpOdI |
| 38. | FRANCIS JOSEpH COSMAS |
| 39. | FUHIAMENI WILLY KISHIMBO |
| 40. | FULgENCE pETER KASANdA |
| 41. | gEOFREY gAMALIEL KANZA |
| 42. | gERALdINE KOKWENdA MWIJAgE |
| 43. | gERVAS ANICETH BAKWASA |
| 44. | gERVAS JOSEpH KAVISHE |
| 45. | gLORIA dOMINIC gANdYE |
| 46. | gOVERNMENT EMpLOYEES pROVIdENT FUNd |
| 47. | gRACE HILARY MBIRIgENdA |
| 48. | HAdIJA ABdALLAH KALLI |
| 49. | HAMIdA AdAM LASHIKONI |
| 50. | HAMIdA AdAM LASHIKONI |
| 51. | HAROUN dAUSON MWAKIBETE |
| 52. | HEAVENS EdEN MREMA |
| 53. | HENRY JOHN CHACKY |
| 54. | IRENE SAMUEL MJATA |
| 55. | JACOB MARTIN MULIKUZA |
| 56. | JAIROS YAHYA FWIMI |
| 57. | JALIBU MRISHO JALIBU MWENEMILAO |
| 58. | JAMES gOdFREY MKUMBO |
| 59. | JAMES MALEMBEKA KASEMBO |
| 60. | JANE ARTHUR MASANJE |
| 61. | JApHET RAZIEL NYAMBO |
| 62. | JAYESH pRAVIN gANATRA |

| | |
|---|---|
| 63. | JIMMY ANdREW YONA |
| 64. | JOAN JULIUS MALINgUMU |
| 65. | JOSEpH ALISONATHAN KELYA |
| 66. | JOSEpH CHARLES BUNdALA |
| 67. | JOYCE MdOE SHAIdI |
| 68. | JUMA BAKARI MUSSA |
| 69. | JUMApILI ABdALLAH KHALIKI |
| 70. | KASAMANgWA ALEX SENEdA |
| 71. | KASIMU ABdALAH UgAMA |
| 72. | KINONI AdAM WAMUNZA |
| 73. | LILIAN KALEB MAKUNdI |
| 74. | LOVENESS YOAS KAYEMA |
| 75. | LYdIA AggREY MWAIJANdE |
| 76. | MARgARET STEpHEN BUBERWA |
| 77. | MARIA WILLY MWIdETE |
| 78. | MARTIN ANTHONY MSEY |
| 79. | MARY dIdAS KEREpI |
| 80. | MARY gEOFREY KANZA |
| 81. | MARY ISSA MUSHI |
| 82. | MICHAEL SIMON MTAMA |
| 83. | MNAZI MMOJA pRIMARY SCHOOL 1990 gROUp |
| 84. | MORAVIAN KARIAKOO SACCOS |
| 85. | MpOKI JOHN MWAIKOKESYA |
| 86. | MWANAIdI SELEMANI JABIRI |
| 87. | MWANAMVUA ALMASSY HASSAN |
| 88. | NANCY ROWLANd SWAI |
| 89. | NAOMI SAMUEL MAKAMBA |
| 90. | NASIBU OMARY MTULWA |
| 91. | NOAH JORAM NZAWILA |
| 92. | NOBERT SHIRIMA |
| 93. | ONESMO RICHARd NdAKI |
| 94. | pATRICK FRANCIS MASINdA |
| 95. | pAULO KULWA NgUMIJI |
| 96. | pETER CYpRIAN NgILIULE |
| 97. | pONTIAN BENEdICT RWEYEMAMU |
| 98. | RASHId MRISHO RASHId |
| 99. | ROgERS LWITIKO MWAKALUKWA |
| 100. | ROSEMARY NIYO BgOYA |
| 101. | RUgINA BELLEN RUgINA |
| 102. | RUKIA CHIKAULA MILLANZI |
| 103. | RUTH BURRA gEAY |
| 104. | SAIdI CHARLES CHIWANgO |
| 105. | SAMIA ISSHACKY ALLY |
| 106. | SHAIBU MBWANA MWAMBUNgU |
| 107. | SOpHIA RICHARd MgAYA |
| 108. | STELLA SAMUEL FUMBUKA |
| 109. | THECLA JAMES MAgUHA |
| 110. | TWALIBU MUSA CHOgA |
| 111. | VERONICA ROCHUS KANWERA |
| 112. | WILBAFOS JULIUS KIRUMBA |
| 113. | WILSON ZAKARIA SIRIKWA |
| 114. | YAHYA SHAABAN RAJABU |
| 115. | ZAINAB AHMEd SAgHEIR |

Jikimu Income Scheme
LIVE WELL ...YOU DESERVE IT

# 3 Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili

**Hakukuwa na yatokanayo na Mkutano Mkuu uliopita wa Mfuko wa Jikimu**

Jikimu Income Scheme
Live Well ...You Deserve It

# TAARIFA FUPI YA MWAKA YA MFUKO WA JIKIMU


Jikimu Income Scheme
Live Well ...You Deserve It

# 4 Barua ya Mwenyekiti wa Bodi

# BARUA YA MWENYEKITI KWA WAWEKEZAJI WA MFUKO WA JIKIMU KWA MWAKA 2025

**Ndugu Wawekezaji,**

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ninayo furaha kuwakaribisha nyote katika Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu (13) wa Mfuko wa Jikimu Tunawashukuru kwa kutenga muda wa kuhudhuria mkutano huu ambao utajadili maendeleo ya Mfuko kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2025.



Ndugu wawekezaji, nina imani mmekuwa mkifuatilia maendeleo ya Mfuko na kwamba mmeipokea, kuipitia na kuichambua taarifa ya Mfuko kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2025. Ninayo furaha kuwajulisha kuwa utendaji wa mfuko kwa kipindi hicho umeendelea kuwa mzuri na wakuvutia. Faida kwa wawekezaji ilikuwa kubwa ikilinganishwa na kigezo linganifu (performance Benchmark). Faida kwa mwaka ilikuwa asilimia 15.5 ikilinganishwa na asilimia 13.7 ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Faida iliyopatikana imeenda sambamba na maendeleo ya soko la fedha na ni kubwa kuliko kigezo linganifu cha asilimia 12.1. Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia Juni 2025, thamani ya mfuko iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 26.8 iliyofikiwa tarehe 30 Juni 2024 hadi Shilingi bilioni 38.5 tarehe 30 Juni 2025. Ongezeko la thamani ya Mfuko limetokana na faida nzuri iliyopatikana pamoja na kuongezeka kwa uelewa juu ya faida zinazopatikana katika Mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

## Mwenendo wa Uchumi na Mazingira katika Soko la Fedha

Ndugu wawekezaji, kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, hali ya uchumi nchini Tanzania imeendelea kuimarika. Pato la Taifa (Gross Domestic Product) lilikua kwa asilimia 5.5 kwa mwaka 2024 na inategemea kukua kwa asilimia 6.0 kwa mwaka 2025. Kiwango hiki cha ukuaji uchumi unaifanya nchi ya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki na za Ukanda wa Ushirikiano wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambazo Uchumi wake unakua vizuri. Kwa mujibu wa taarifa za Benki Kuu ya Tanzania, mfumuko wa bei ulikuwa kati ya asilimia 3.0 hadi 3.3 kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 June 2025, ikilinganishwa na matarajio ya kiwango cha kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0. Kiwango hiki pia kimeendana na matarajio ya nchi za ukanda wa Afrika Mashariki cha asilimia 8 na kiwango cha kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0 kwa nchi za SADC. Kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioishia tarehe 30 Juni 2025, viwango vya riba katika soko havikubadilika sana na hivyo kuashiria utulivu wa soko kwa ujumla. Kwa upande mwingine, thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani ilibaki kuwa imara ambapo iliimarika kwa kiwango kidogo cha asilimia 0.3.

Kuhusu Soko la Mitaji na Dhamana, maendeleo mazuri yameshuhudiwa katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 June 2025. Mtaji katika soko la hisa la Dar es Salaam umeongezeka kwa asilimia 16.7 kutoka kiasi cha shilingi trillioni 16.8 tarehe 30 June 2024 hadi trilioni 19.6 tarehe 30 Juni 2025. Pia, bei ya Hisa zilizoorodheshwa zimeongezeka kama inavyo onyeshwa na Fahirisi (Tanzania Share Index). Katika kipindi cha mwaka kilichoishia tarehe 30 Juni 2025, kumekuwa na ongezeko la Fahirisi la asilimia 8.4 ambapo iliongezeka toka 4,475.20 tarehe 30 Juni 2024 hadi 4,852.30 tarehe 30 Juni 2025. Hali hii inaonyesha kwamba, katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2025, bei za hiza kwa ujumla ziliongezeka. Sababu za kupanda kwa bei za Hisa kulichagizwa na kufanya vyema kwa Makampuni yaliyoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na kuongezeka kwa imani ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji hapa nchini. Tunaishukuru Serikali kwa ujumla kwa kuendelea kuweka mazingira bora ya biashara na usimamizi nchini

## Utendaji wa Mifuko na Maendeleo Mengineyo

Ndugu Wawekezaji, kuhusu utendaji wa Mifuko kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2025, viashiria vya kiuchumi vinaonyesha kwamba, Kampuni ya UTT AMIS pamoja na Mifuko inayoisimamia imeendelea kufanya vizuri. Thamani ya Mifuko imeongezeka kutoka Shilingi Trilioni 2.2382 mnamo tarehe 30 Juni 2024 hadi kufikia Shilingi Trilioni 3.2687 tarehe 30 Juni 2025. Hili ni ongezeko la shilingi 1.0305 trilion sawa na asilimia 46.0 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 702.8, sawa na asilimia 45.7 kwa mwaka uliotangulia. Ongezeko la ukubwa wa Mifuko limetokana na ongezeko la idadi ya Wawekezaji 143,990, sawa na asilimia 44.0 waliojiunga katika Mifuko kwa mwaka 2025, ikilinganishwa na Wawekezaji 79,519, sawa na asilimia 32.0 waliojiunga mwaka wa fedha uliotangulia. Kama nilivyosema hapo awali kwamba mifuko yote imetoa faida nzuri kwa wawekezaji wake.

Ndugu Wawekezaji, katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2025, Kampuni ya UTT AMIS iliendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati mpya wa miaka mitano. Awali, Mpango huu ulipangwa kuhitimishwa katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2029 lakini baadae ulifanyiwa marejeo na sasa utakamilika mwezi Juni, 2030 ili kuendana na mpango wa Serikali. Katika Mpango

Mkakati Mpya, Kampuni ya UTT AMIS inatarajia kukuza uwekezaji katika Mifuko kutoka shilingi Trilion 2.2 tarehe 30 June 2024 hadi Shilingi Trilioni 8.5 tarehe 30 June 2030. Zaidi ya hapo, miongoni mwa malengo ya taasisi ni pamoja na kuendelea kutoa huduma za kidijitari huku ikiongeza idadi ya vituo vya huduma kwa wateja ili kusogeza zaidi huduma kwa wawekezaji. Kama ambavyo mmeshuhudia, UTT AMIS imekamilisha maboresho ya Mfumo wa kisasa wa kutolea huduma. Mfumo huu utaruhusu uchakataji wa miamala mingi zaidi kwa wakati, kupatikana kwa huduma mbalimbali na hivyo wawekezaji kufurahia huduma zitolewazo na UTT AMIS. Kampuni ya UTT AMIS itaendelea kuuelimisha umma juu ya huduma za kidijitali zinazopatikana katika mfumo mpya.

## Matarajio ya mwaka wa fedha 2025/2026

Ndugu Wawekezaji, kwa kipindi cha mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa UTT AMIS unaoishia Juni 2030 umewezesha thamani ya mifuko kufikia Shilingi trilioni 3.27 ukilinganisha na matarajio ya ukuaji wa hadi trilioni 2.79. Ukuaji huu unatoa msingi wa kuyafikia malengo ya thamani ya mifuko. Kwa kuzingatia mageuzi ambayo kampuni ya UTT AMIS inayatekeleza, maendeleo ya sasa katika soko na mazingira bora ya biashara ambayo yamefanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimatumaini yetu kuwa mifuko itaendelea kutoa faida nzuri kwa wawekezaji huku ikiendelea na uboreshaji wa uendeshaji na utoaji huduma kwa wateja ili kusaidia juhudi za ukuzaji wa mitaji kwa wawekezaji.

## Dira ya Maendeleo 2050

Maendeleo ya miaka 25 hadi 2050 yenye lengo mahsusi la kukuza pato la Nchi kutoka Dola za Kimarekani Bilioni 85 za sasa hadi Dola Trilioni Moja kiasi ambacho ni takribani mara kumi na mbili. Njia mojawapo ya kuweza kufikia lengo hilo ndani ya kipindi cha miaka ishirini na tano ijayo ni kuendelea kuwekeza akiba yako katika mifuko ya UTT AMIS. Nipende kukuhakikishia kuwa uwekezaji wa UTT AMIS unafanywa kwa weledi na wataalamu wetu katika maeneo ambayo ni salama na yenye tija chini ya usimamizi wa Bodi ya Wakurugenzi na Mamlaka za usimamizi za Umma kama vile Mamlaka ya Usimamizi wa Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Benki Kuu ya Tanzania. Kama Mwekezaji, umefanya uamuzi sahihi wa kuwekeza katika mifuko ya Uwekezaji wa pamoja kama vile Mfuko wa **Jikimu.** Uamuzi huo ni njia nzuri ya kutawanya fedha zako katika uwekezaji anuai huku ukifurahia maajabu ya Kampaundi. Hii itakufanya uendelee kupata faida ukiwa umelala au unaendelea na shughuli nyingine. Aidha, inatupasa kuzingatia ushauri wa aliyekuwa Mfanyabiashara Maarufu, marehemu billionea Charlie Munger, ya kwamba “Usikatize uwekezaji wako bila ya kulazimika kufanya hivyo” kwa maneno mengine, utanufaika na maajabu ya Kampaundi endapo uwekezaji wako utakaa kwa muda mrefu pasipo kuuza vipande vyako. Hii ni mojawapo ya njia ya uhakika ya kujitengenezea utajiri endelevu kwa manufaa yako binafsi na kwa jamii na hivyo kushiriki kikamilifu katika kusaidia taifa kulifikia lengo la pato la Dola za Kimarekani trilioni moja.

## Shukrani

Ndugu Wawekezaji, Kwa kuhitimisha, napenda niwashukuru nyote kwa ushirikiano na imani yenu kwa UTT AMIS na Mfuko wa Jikimu kwa kipindi chote cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2025. Kwa namna ya kipekee nipende kuishukuru Serikali kupitia Wizara ya Fedha,Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Msimamizi wa Mifuko ambaye ni Benki ya CRDB, Soko la Hisa la Dar es Salaam pamoja na Madalali wake, Wajumbe wenzangu wa Bodi ya Wakurugenzi, Wafanyakazi wa UTT AMIS na Wadau wote ambao wameendelea kuiwezesha UTT AMIS kutekeleza majukumu yake katika mwaka huu wa fedha. Ni matumaini yangu kuwa ushirikiano huu utaendelea kwa manufaa ya Wawekezaji wetu na maendeleo ya Soko la Mitaji na Sekta ya Fedha hapa Nchini kwetu.



Prof. Faustin Rweshabura Kamuzora
**Mwenyekiti wa Bodi**

# 5 Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko wa Jikimu

**CRDB BANK PLC**
Makao Makuu: Barabara ya Ally Hassan
Mwinyi / Barack Obama
S.L.P. 268, Dar es Salaam - Tanzania
Simu: +255 (0) 22 211 7441-7
Nukushi: +255 (0) 22 211 6714
Barua pepe: info@crdbbank.co.tz
Tovuti: www.crdbbank.co.tz

# TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO WA JIKIMU KWA WAWEKEZAJI

Tukiwa ni waangalizi wa Mfuko wa **Jikimu**, Jukumu letu ni kusimamia kwamba utendaji wa meneja wa mfuko unaendana/ unazingatia waraka wa makubaliano ili kuhakikisha maslahi bora ya wenye vipande. Katika utekelezaji wa kazi hii, mwangalizi wa mfuko ana majukumu yafuatayo; Uangalizi wa mali za mfuko, kuhakikisha meneja wa mfuko anatumia njia/mbinu sahihi katika kukokotoa mahesabu ya thamani ya mfuko sambamba na mkataba wa makubaliano, na pia kuhakikisha viwango vya uwekezaji vinazingatiwa.

Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, kilichoanzia tarehe 01.07.2024 mpaka 30.06.2025, Benki ya CRDB kama mwangalizi wa mfuko wa **Jikimu**, tumeendeleza uangalizi wa mwenendo wa shughuli za meneja wa mfuko, utekelezaji wake na kuangalia changamoto kwenye uwekezaji.

Kwa kuzingatia hayo, tunapenda kuwathibitishia kwamba shughuli za uwekezaji kwenye mfuko wa **Jikimu** na wajibu wa meneja wa mfuko (UTT AMIS), vimeendeshwa/ vimetekelezwa kufuatana na vipengele vya waraka wa makubaliano. Tukizingatia suala la imani/ uaminifu wa wenye vipande kwenye mfuko, tunathibitisha kwamba maslahi ya wenye vipande ndani ya mfuko wa **Jikimu** yanalindwa na kuzingatiwa ipasavyo, na meneja ameendesha mfuko kulingana na waraka wa makubaliano.

*Abdulmajid M. Nsekela*

**Afisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji** **Tarehe:** Novemba, 2025

# 6 Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko

# TAARIFA YA MKAGUZI KUHUSU MUHTASARI WA HESABU ZA MFUKO WA JIKIMU (JIKIMU FUND)

KPMG

Jengo la Luminary

Ghorofa ya 2, Kitalu Na. 574

Barabara ya Haile Selassie, Msasani

S. L. P. 1160, Dar es Salaam

Simu: +255 22 2600330

Barua Pepe: info@kpmg.co.tz

Tovuti: www.kpmg.co.tz

***Maoni***

Muhtasari wa hesabu za Mfuko ambao unajumuisha muhtasari wa Urari wa hesabu za Mfuko mnamo tarehe 30 Juni 2025, muhtasari wa Mapato na Matumizi, muhtasari wa Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko pamoja na muhtasari wa Mtiririko wa Fedha umetayarishwa kutoka katika taarifa kamili ya ukaguzi ya Mfuko wa Jikimu kwa kipindi cha mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2025.

Kwa Maoni yetu, Muhtasari wa Hesabu za Mfuko wa Jikimu unaendana na taarifa kamili ya hesabu za Mfuko zilizokaguliwa kulingana na vigezo vilivyoelezwa kwenye dokezo namba 1.

***Muhtasari wa Taarifa ya Hesabu za Fedha***

Muhtasari wa taarifa ya hesabu za fedha haioneshi taarifa zote kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha kama ilivyotolewa na Bodi ya Kimataifa ya usimamizi wa viwango vya utoaji taarifa za fedha (International Accounting Standard Board (IFRS Accounting Standards)). Muhtasari huu wa hesabu pamoja na hii taarifa yetu siyo mbadala wa taarifa kamili ya hesabu za kifedha iliyokaguliwa. Muhtasari wa hesabu za kifedha pamoja na taarifa kamili ya hesabu zilizokaguliwa haijumuishi matukio au miamala baada ya tarehe za taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa.

***Taarifa ya Ukaguzi na Hesabu za Fedha zilizokaguliwa***

Maoni ya ukaguzi (audit opinion) yasiyokuwa na kasoro juu ya taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha za Mfuko yalitolewa kwenye taarifa ya tarehe 20 Novemba 2025 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2025.

Taarifa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2025 inajumuisha mambo mengine Muhimu juu ya ukaguzi wa hesabu za mfuko.

***Majukumu ya Meneja Kuhusu Muhtasari wa Hesabu za Fedha za Mfuko***

Meneja wa Mfuko anahusika na utayarishwaji wa muhtasari wa hesabu za fedha za Mfuko kwa mujibu wa vigezo kama ilivyoainishwa kwenye dokezo namba 1.

***Majukumu ya Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko***

Majukumu yetu kama wakaguzi wa hesabu za Mfuko ni kutoa maoni kama muhtasari wa hesabu za Mfuko unaendana na taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha na kwa mujibu wa taratibu zetu za ukaguzi, ukaguzi ambao ulifanywa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi (International Standards on Auditing-ISA) 810 (kama ilivyorekebishwa), “Kazi za kuripoti juu ya Muhtasari wa taarifa za kifedha”

**Hili ni toleo lililotafsiriwa la ripoti ya Mkaguzi liyosainiwa katika toleo la Kiingereza.**

## Dokezo juu ya vigezo vya kutayarisha Muhtasari wa Hesabu

Muhtasari wa taarifa ya hesabu za fedha umetayarishwa kutoka kwenye taarifa kamili ya ukaguzi, iliyotayarishwa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha (IFRS) mnamo tarehe 30 Juni 2025.

Taratibu za kutayarisha muhtasari wa hesabu za fedha unaitaka menejimenti kuamua kiwango cha taarifa zitakazojumuishwa katika muhtasari ili kuendana kwa kiwango kikubwa na taarifa kamili ya ukaguzi au kutoa taswira ya muhtasari iliyosawa na taarifa ya hesabu za fedha zilizo kaguliwa

Menejiment imetayarisha hesabu hizi kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

(a) Muhtasari wa Hesabu unajumuisha hesabu zote za mfuko zilizoko katika taarifa ya hesabu zilizokaguliwa;

(b) Taarifa zilizopo kwenye muhtasari wa hesabu zinashabihiana na taarifa ya hesabu za mfuko zilizokaguliwa na

(c) Jumla kuu, jumla ndogo pamoja na taarifa linganifu zilizopo kwenye hesabu zilizokaguliwa zimeonyeshwa pia katika muhtasari wa hesabu ulioandaliwa

Taarifa ya hesabu za Mfuko wa Jikimu zilizokaguliwa zinapatikana katika ofisi ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT (UTT AMIS).

Jikimu Income Scheme
Live Well ...You Deserve It

# 7 Taarifa ya Hesabu za Mfuko

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI (Statement of Profit or Loss and Other Comprehensive Income) KWA MWAKA UNAOISHIA 30 JUNI 2025

| | 2025<br>TSH'000 | 2024<br>TSH'000 |
|---|---:|---:|
| Mapato yatokanayo na Uwekezaji | 4,057,444 | 2,607,982 |
| Faida/(hasara) kwenye uthamini wa mali za kifedha | 710,830 | 363,380 |
| Mapato mengineyo | 1,089,527 | 1,014,686 |
| **Jumla ya Mapato** | **5,857,801** | **3,986,048** |
| Gharama za Meneja | (579,370) | (412,462) |
| Gharama za Mwangalizi wa Mfuko | (32,187) | (22,915) |
| Gharama za Mauzo ya Dhamana na Hisa | (17,226) | (14,842) |
| Gharama za Ukaguzi wa Hesabu | (2,531) | (2,459) |
| Gharama za Mauzo ya Vipande | (224,532) | (153,174) |
| Gharama nyinginezo za Uendeshaji | (61,541) | (38,850) |
| **Jumla ya Gharama za uendeshaji** | **(917,387)** | **(644,702)** |
| **Mapato kabla ya gawio kwa wenye Vipande** | **4,940,414** | **3,341,346** |
| Gawio la mapato kwa wenye vipande | (2,188,534) | (1,668,561) |
| **Ongezeko la Thamani (Mapato) Kwa Wakezaji Kabla ya Kodi** | **2,751,880** | **1,672,785** |
| Kodi | (74,678) | (26,483) |
| **Ongezeko la Thamani (Mapato) Kwa Wakezaji Baada ya Kodi** | **2,677,202** | **1,646,302** |
| Mapato mengineyo(other comprehensive income) | - | - |
| **Ongezeko halisi la thamani ya Mfuko** | **2,677,202** | **1,646,302** |

## URARI WA HESABU ZA MFUKO (BALANCE SHEET)
## MNAMO TAREHE 30 JUNI 2025

| | 2025<br>TSH'000 | 2024<br>TSH'000 |
|---|---|---|
| **Rasilimali za Mfuko** | | |
| Fedha Taslim | 4,505,908 | 5,528,665 |
| Dhamana za Serikali | 27,813,073 | 15,332,038 |
| Uwekezaji Katika Hisa | 6,678,535 | 6,275,370 |
| Rasilimali nyinginezo (other receivable) | 70,495 | 18,942 |
| **Jumla ya Rasilimali** | **39,068,011** | **27,155,015** |
| | | |
| **Dhima ya Mfuko** | | |
| Dhima Nyinginezo | (1,119,497) | (951,776) |
| **Jumla ya Dhima ya Mfuko** | **(1,119,497)** | **(951,776)** |
| **Thamani Halisi ya Mfuko** | **37,948,514** | **26,203,239** |
| | | |
| **Inawakilishwa na:** | | |
| **Thamani Halisi ya Mfuko** | **37,948,514** | **26,203,239** |
| **Idadi ya Vipande** | **201,318,654** | **151,598,376** |
| **Thamani ya Kipande** | **188.50** | **172.85** |

# TAARIFA YA MABADILIKO YA THAMANI YA MFUKO (STATEMENT OF CHANGES IN NET ASSETS ATTRIBUTABLE TO UNIT HOLDERS) KWA MWAKA ULIOSHIA 30 JUNI 2025

| | 2025<br>TSH'000 | 2024<br>TSH'000 |
|---|---:|---:|
| **Thamani ya mfuko  mwanzoni mwa mwaka(Julai 1)** | **26,203,239** | **19,343,073** |
| Mabadiliko/Ongezeko ya thamani ya mfuko | 2,677,202 | 1,646,302 |
| | **28,880,441** | **20,989,375** |
| **Miamala (Transactions) ya wenye vipande kwa mwaka** | | |
| Mauzo ya vipande (Sales) | 12,948,614 | 9,067,304 |
| Ununuzi ya vipande (Repurchase) | (3,880,541) | (3,853,440) |
| **Mabadiliko ya thamani ya mfuko** | **9,068,073** | **5,213,864** |
| **Thamani halisi ya Mfuko** | **37,948,514** | **26,203,239** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA (CASH FLOW STATEMENT) KWA MWAKA UNAOISHIA 30 JUNI 2025

| | 2025<br>TSH'000 | 2024<br>TSH'000 |
|---|---|---|
| **FEDHA ITOKANAYO NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | |
| Ongezeko la Thamani (Mapato) Kwa Wawekezaji baada ya Kodi | **2,677,202** | **1,646,302** |
| **Imerekebishwa na:** | | |
| Gawio kwenye hisa | (467,257) | (326,637) |
| Faida itokanayo na mabadiliko ya thamani ya dhamana | (710,830) | (363,380) |
| Gawio kwa wenye vipande | 2,188,534 | 1,668,561 |
| Kodi ya zuio | 74,678 | 26,483 |
| Faida itokanayo na mauzo ya dhamana | (976,820) | (942,848) |
| Mapato yatokanayo na riba (effective interest rate method) | (3,590,187) | (2,281,345) |
| **Fedha iliyopatikana kabla ya mabadiliko ya Mtaji wa uendeshaji:** | **(804,680)** | **(572,864)** |
| Mabadiliko ya Mtaji wa uendeshaji | | |
| Ongezeko /(Kupungua) kwa Dhamana za serikali | (10,884,983) | (792,522) |
| Ongezeko /(Kupungua) kwa uwekezaji kwenye Hisa | 307,665 | (322,000) |
| Ongezeko /(Kupungua) kwa dhima ambazo mfuko haujalipwa | (35,055) | 28,519 |
| Ongezeko /(Kupungua) kwa dhima ambazo mfuko haujalipa | (840,347) | (538,997) |
| **Fedha iliyopatikana kutoka kwenye shughuli za uendeshaji** | **(12,257,400)** | **(2,197,864)** |
| Mapato yaliyopokelewa kutokana na uwekezaji katika hisa | 450,759 | 314,662 |
| Mapato yaliyopokelewa kutokana na riba | 2,970,955 | 2,485,639 |
| Kodi iliyolipwa hadi sasa | (74,678) | (26,483) |
| Fedha halisi itokanayo na shughuli za uendeshaji | **(8,910,364)** | **575,954** |
| **AMANA YA MFUKO (FINANCING ACTIVITIES)** | | |
| Mauzo ya Vipande (Sales of Units) | 12,948,614 | 9,067,304 |
| Ununuzi (Repurchase) wa Vipande | (3,880,541) | (3,853,440) |
| Gawio lililolipwa | (1,180,466) | (965,466) |
| **Fedha halisi iliyotumika kutokana na miamala ya wenye vipande** | **7,887,607** | **4,248,398** |
| Ongezeko/(Punguzo) halisi la Fedha | (1,022,757) | 4,824,352 |
| Salio la fedha mwanzoni mwa Mwaka | 5,528,665 | 704,313 |

....................................
**Mwenyekiti wa Bodi**
**Tarehe:** Novemba, 2025

....................................
**Mkurugenzi**
**Tarehe:** Novemba, 2025

# 8 Taarifa ya Meneja kuhusu Uwekezaji

Jikimu Income Scheme
LIVE WELL ...YOU DESERVE IT

# Taarifa ya Meneja Kuhusu Uwekezaji


Mfuko wa Jikimu ni mfuko wa wazi ulioanzishwa kwa lengo la kuwasaidia wawekezaji kupanga na kujipatia mapato ya mara kwa mara kwa ajili ya kukidhi gharama za maisha huku wakifaidika na ongezeko la mtaji katika uwekezaji wao. Mfuko unampatia mwekezaji fursa ya kuchagua mojawapo kati ya aina tatu za mpango wa uwekezaji (a) Gawio la kila robo mwaka (b) Gawio la kila mwisho wa mwaka (c) Kukuza mtaji.

## 1.0 Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2025, mfuko wa Jikimu ulikuwa na ukubwa wa shilingi bilioni 38.5. Aidha, kwa kipindi cha mwaka mmoja ukubwa wa Mfuko umeongezeka kwa shilingi bilioni 11.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.8 mwaka 2024.

Thamani ya kipande imeongezeka kwa shilingi 18.0 hadi kufikia shilingi 191.8.

*Chati Na. I; Ukuaji Wa Mfuko Wa Jikimu Kutoka Kuanzishwa Hadi tarehe 30 Juni, 2025*





Aidha, tangu mfuko uanzishwe umefanikiwa kulipa wawekezaji gawio lenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 17.0.

## 2.0 Mgawanyo wa Uwekezaji

Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 mwezi Juni 2025, UTT-AMIS PLC kama meneja wa Mfuko alitumia uzoefu na weledi katika kufikia mgawanyo anuai wa rasilimali kwa matakwa ya sera za mfuko wa Jikimu. Mgawanyo anuai wa rasilimali za mfuko mwezi Juni 2025 ulikuwa kama inavyoonekana kwenye chati namba II hapo chini:-

*Chati Na. II: Mgawanyo wa Uwekezaji wa Mfuko wa Jikimu hadi tarehe 30 Juni 2025*




Chati namba II, inaonesha mgawanyo wa uwekezaji katika mfuko wa Jikimu ambapo asilimia 72.04 imewekezwa katika Dhamana za Serikali za muda mrefu, ikifuatiwa na asilimia 17.28 kwenye hisa, huku amana za benki za muda maalumu ikiwa ni asilimia 10.66, asilimia 0.02 kwenye Amana za benki za muda mfupi. Aidha, Chati hiyo inaonesha kiwango kikubwa cha asilimia kimewekezwa kwenye Dhamana za Serikali za muda mrefu ili kuimarisha kiwango cha faida na mapato ya Mfuko.

**KUANZISHWA;**

**OKTOBA, 2008**

**30 JUNI 2025**

**THAMANI YA KIPANDE SHILINGI 191.8**

**UKUBWA WA MFUKO SHILINGI BILIONI 38.5**

**GAWIO KWA KILA KIPANDE KWA MWAKA SHILINGI 12.0**

**FAIDA KWA MWAKA 15.5%**

## 3.0 Faida

Kiwango cha faida kwa kipindi cha mwaka mmoja ni asilimia 15.5 ikilinganishwa na faida ya asilimia 13.7 mwaka 2024. Aidha, kiwango cha faida kwa mwaka 2025 cha asilimia 15.5 ni zaidi ya kigezo cha ufanisi cha asilimia 12.1 kama inavyonekana kwenye (Jedwali I).

Jedwali namba I na II, linaonesha mwenendo wa utendaji wa Mfuko pamoja na kigezo cha ufanisi (benchmark) kwa mwaka 2021 hadi 2025. Hali ya utendaji wa Mfuko inaonekana ni nzuri na shindani ikilinganishwa na faida ya kigezo cha ufanisi na maeneo linganifu sokoni.

***Jedwali Na I: Faida ya Mfuko wa Jikimu tangu Juni, 2021 hadi Juni, 2025***

| Na. | Mwaka wa Fedha | Ukubwa wa mfuko Shilingi Bilioni | Hali ya Utendaji | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Faida | Kigezo cha ufanisi |
| 1.0 | 2025/25 | 38.5 | 15.5% | 12.1% |
| 2.0 | 2023/24 | 26.8 | 13.7% | 11.2% |
| 3.0 | 2022/23 | 20.0 | 13.6% | 7.6% |
| 4.0 | 2021/22 | 18.5 | 13.6% | 8.7% |
| 5.0 | 2020/21 | 17.9 | 18.8% | 8.1% |

*Kumb:kigezo cha ufanisi ni mjumuiko wa utendaji wa Fahilisi za hisa kwa kampuni za ndani (TSI) na faida kwenye Dhamana ya Serikali ya miaka 10.*

Ili kupima mafanikio ya mfuko inabidi kulinganisha na viwango vya faida vinavyotolewa na soko kwenye Amana za benki na Dhamana za Serikali kama vinavyoonekana kwenye Jedwali namba II hapo chini:

***Jedwali Na. II: Viwango vya faida katika Dhamana za Serikali na Amana za benki***

| Maelezo | Kwa Mwaka Wa Fedha Ulioisha Mwezi Juni | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 10 | 10.3% | 11.1% | 12.3% | 14.2% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 7 | 9.3% | 9.7% | 9.7% | 9.7% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 5 | 8.9% | 9.7% | 10.0% | 12.9% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 2 | 4.4% | 9.1% | 11.6% | 12.0% |
| Dhamana ya Serikali ya Mwaka 1 | 4.7% | 6.9% | 8.3% | 8.8% |
| Amana za benki | 1.5% | 1.6% | 2.8% | 2.9% |

*Chanzo; Benki Kuu ya Tanzania*

Mambo mengine muhimu ya kuzingatia wakati wa kulinganisha faida za uwekezaji katika Mfuko wa Jikimu na amana katika benki;

- Viwango vya faida vinavyooneshwa hapo juu kwa uwekezaji chini ya miaka mitatu ni kabla ya kutoa kodi ya zuio (withholding tax) ya 10% wakati faida ya mfuko wa Jikimu ni baada ya kutoa kodi ya zuio ya 10% na gharama zingine.
- Mfuko wa Jikimu unaruhusu wanachama wake kuuza vipande vyao (hulipwa ndani ya siku kumi (10) za kazi) wakati wowote hivyo kumpa fursa mwekezaji kupata fedha pindi anapozihitaji na kwamba hakuna kiwango cha chini cha uwekezaji kisichopata faida.
- Viwango vya faida kwenye mfuko vinatolewa sawa kwa wawekezaji wote (wawekezaji wa kipato kidogo, wa kipato cha kati na wale wenye kipato kikubwa).
- Mfuko wa Jikimu hutoa gawio kwa wawekezaji wake kila robo mwaka na kwa mwaka
- Urahisi wa kuongeza na kutoa fedha, aidha mtu anaweza kununua na kuuza vipande .
- Kuwekeza kwenye mfuko wa Jikimu kuna faida zaidi ya kuwa na akaunti ya amana kwa sababu inamuongezea mwekezaji kipato kikubwa kutokana na viwango bora vya faida vinavyotolewa na mfuko zaidi ya viwango vya faida kwenye amana.

## 4.0 Mwenendo wa Uchumi, Tanzania

### 4.1 Pato la Taifa

Kwa mwaka 2024, uchumi wa Tanzania unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.5 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.0 mwaka 2025. Ukuaji huu wa asilimia 5.5 ni mkubwa ukilinganishwa na asilimia 5.1 iliyonakiriwa mwaka 2023. Kwa mujibu wa Ripoti ya Uhimilivu wa Kifedha iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania, mafanikio haya yamechangiwa na mambo kadhaa, ikiwa ni pamoja na muendelezo wa utekelezwaji wa miradi ya kimkakati ya miundombinu na juhudi za serikali za kuboresha mazingira ya uwekezaji.

*Jedwali Na. III: Mwenendo wa ukuaji wa Pato Halisi la Taifa*

| Mwaka | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Pato halisi la Taifa | 7.0% | 4.8% | 4.9% | 4.7% | 5.1% | 5.5% | 6.0%* |

Ongezeko chanya la ukuaji wa uchumi linaloonekana tangu mwaka 2022 linaashiria kuwa biashara na shughuli za maendeleo zimefanya vizuri. Aidha, viashiria vinaonyesha kuwa kiwango cha uwekezaji na shughuli sokoni viliongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita. Soko la mitaji na dhamana limeshuhudia kuongezeka kwa wasimamizi wapya wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja na kuwepo kwa fursa mpya za Uwekezaji ambazo ziliwavutia wawekezaji kwa kiwango zaidi ya matarajio.

Mwaka 2025, kiasi na thamani ya miamala imeongezeka ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka uliopita. Kwa upande wa mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS, uwepo wa mwenendo mzuri sokoni umeifanya mifuko hiyo kuwa ya kuvutia zaidi sokoni.

### 4.2 Mfumuko wa Bei

Jedwali la IV linaonyesha kuwa kiwango cha mfumuko wa bei kimeendelea kuwa stahimilivu. Kwa mujibu wa Taarifa ya Sera ya Fedha iliyotolewa na Benki Kuu mwezi Julai 2025, kiwango hicho kimeendelea kuwa chini ya kigezo linganifu, cha asilimia 5.0 kilichowekwa na wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Nchi ya Tanzania imefanikiwa kudumisha kiwango cha mfumuko wa bei chini ya kigezo linganifu kwa kipindi cha miaka saba mfululizo, kama inavyooneshwa katika Jedwali Na IV. Mamlaka zimekadiria kuwa katika kipindi cha muda wa kati ya miaka mitatu hadi mitano ijayo, mfumuko wa bei utaendelea kubaki chini ya kiwango cha kigezo linganifu.

Hata hivyo, kufikia tarehe 30 Juni 2025, nchi za Rwanda, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudani Kusini na Burundi zilinakiri kiwango cha mfumuko wa bei cha juu ya kigezo linganifu.

*Jedwali Na. IV: Viwango vya Mfumuko wa Bei*

| Mwaka (Juni) | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfumuko wa Bei | 3.7% | 3.2% | 3.6% | 4.4% | 3.6% | 3.1% | 3. 3% |

Ustahimilivu wa mfumuko wa bei nchini huleta mazingira rafiki kwa wawekezaji na huchagiza maendeleo ya uchumi kwa ujumla. Hali hii husaidia wawekezaji kwenye mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS kupata thamani inayokusudiwa bila kuathiriwa kwa kiwango kikubwa na ongezeko la bei za bidhaa na huduma pindi wanapolipwa gawio au kutoa fedha. Vilevile kwa UTT AMIS, hali hii husaidia uwekezaji kuwa thabiti, na hivyo husaidia wawekezaji kutimiza malengo yao ya kifedha ya muda mrefu.

### 4.3 Sekta ya Fedha

Sekta ya fedha nchini Tanzania imeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi. Mwaka 2024, jumla ya mali kwenye mfumo wa fedha nchini ziliongezeka kwa shilingi trilioni 13.3 na kufikia shilingi trilioni 88.6, ambayo ni zaidi ya asilimia 44.2 ya Pato la Taifa (GDP).

Sekta ya fedha inajumuisha sekta ndogo zifuatazo: benki, hifadhi ya jamii, mifuko ya uwekezaji wa pamoja na bima. Sekta ya benki inachukua asilimia 70.2 ya jumla ya mali kwenye mfumo wa fedha, ikifuatiwa na hifadhi ya jamii kwa asilimia 24.1, mifuko ya uwekezaji wa pamoja kwa asilimia 3.0, na sekta ya bima kwa asilimia 2.6.

#### 4.3.1 Sekta ya Benki

Katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2025, utoaji wa huduma za kifedha kupitia njia za kidijitali uliendelea kupata mafanikio makubwa katika soko la ndani. Benki za biashara, kwa kushirikiana na kampuni za mitandao ya simu zinazotoa huduma za pesa mtandao, ziliboresha majukwaa yanayowawezesha watanzania kuweka akiba, kuhamisha fedha, kuwekeza, na kupata mikopo kwa njia ya pesa mtandao.

Unganishwaji wa huduma za simu na benki umesaidia jamii kuongeza imani ya matumizi ya huduma kidijitali. Wawekezaji sasa wanaweza kufanya miamala kutoka/kwenda kwenye akaunti zao za benki na za pesa mtandao kama vile M-Pesa, Mixx by Yas, Halopesa, Azam Pesa, Selcom Pesa na Airtel Money.

Kwa mwaka 2024, kiasi na thamani ya miamala iliofanyika kutoka kwenye akaunti za pesa mtandao kwenda Benki (W2B) kilifikia milioni 9.5 na shilingi trilioni 3.6, ikiwa ni ongezeko la asilimia 43.3 na asilimia 32.7 mtawalia.

Kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2024/25, jumla ya rasilimali za sekta ya benki ziliongezeka kwa zaidi ya asilimia 10.0 na kufikia shilingi trilioni 72.4. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mikopo, ukichagizwa na uwepo wa huduma za benki kidijitali. Jumla ya mikopo na gharama za huduma ziliongezeka kutoka shilingi trilioni 37.4 hadi shilingi trilioni 44.1, huku amana za wateja ziliongezeka kwa asilimia 19.7 kutoka shilingi trilioni 40.6 hadi shilingi trilioni 48.6.

Kampuni ya UTT AMIS imeunganisha mifumo yake na Kampuni za Mitandao ya Simu pamoja na benki. Unganishwaji huu, unasaidia kurahisisha huduma za kuweka akiba na kuwekeza kwenye fursa mabalimbali. Wawekezaji wa mifuko ya UTT AMIS wanaweza kununua vipande wanavyokusudia kwa kuhamisha fedha moja kwa moja kutoka kwenye akaunti zao za pesa mtandao au akaunti za benki bila ya wao kutembelea ofisi husika.

UTT AMIS ilipokea jumla ya shilingi trilioni 1.9 kupitia mifumo iliyounganishwa. Vivyo hivyo, wawekezaji waliuza vipande (kutoa pesa) vyenye thamani ya jumla ya shilingi trilioni 1.3 (repurchases), kiasi kilicholipwa moja kwa moja kwenye akaunti zao za benki.

### 4.4 Sekta ya Mawasiliano

Kukua kwa sekta ya mawasiliano nchini kumechangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya soko la mitaji na dhamana, hususani katika huduma za kifedha za kidijitali. Huduma za pesa mtandao kama vile M-Pesa, Mixx by Yas, Halopesa, Azam Pesa, Selcom Pesa, na Airtel Money zimetanua zaidi wigo wa huduma za fedha kwa kuwawezesha watumiaji kuweka akiba, kukopa, na kufanya miamala kwa urahisi zaidi.

Idadi ya laini za simu (mkononi na za mezani) ilifikia milioni 92.7 mwezi Juni 2025, ikiwa ni ongezeko la laini milioni 17.2 kutoka mwaka uliopita. Idadi ya akaunti za pesa mtandao ziliongezeka kwa asilimia 22.0, kutoka milioni 55.7 hadi milioni 68.0. Katika mwaka wa fedha wa 2024/25, idadi ya miamala iliyofanyika kutoka kwenye akaunti za pesa mtandao kwenda UTT AMIS iliongezeka kwa asilimia 26.2, kufikia 276,187, huku thamani ya miamala ikiongezeka kwa asilimia 21.8 hadi shilingi bilioni 86.6.

UTT AMIS kwa kushirikiana na benki za biashara na Kampuni za Mitandao ya Simu (MNOs), imefanikiwa kuunganisha mifumo yake ya malipo na uendeshaji. Wawekezaji sasa wanaweza kufungua akaunti, kujiandikisha, kutoa fedha, na kuona salio kupitia programu tumizi ya UTT AMIS au kwa kupiga msimbo *150*82#. Mwekezaji anaweza kuuza vipande (repurchase) hadi shilingi milioni 5.0 kwa njia ya simu kwa siku.

UTT AMIS inatarajia kuzindua mfumo wa kidijitali kwa wawekezaji kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2025/26. Mfumo huu utatoa uwezo kwa wawekezaji kujihudumia wenyewe kwa kufanya shughuli kama usajili, miamala, mawasiliano, na usimamizi wa akaunti, hivyo kurahisisha uwekezaji. Pia, UTT AMIS imeongeza ofisi mpya katika mikoa ya Morogoro, Kahama na Dar es Salaam, na kufanya jumla ya ofisi nchini kufikia nane (8). Ofisi hizi hutumika kama vituo vya elimu ya kifedha, ushirikiano kwa jamii, na msaada kwa wawekezaji.

### 4.6 Viwango vya Riba na Faida

Wastani wa faida kwa dhamana za serikali za muda mfupi iliongezeka hadi asilimia 8.8 mwezi Juni 2025, kutoka asilimia 8.3 mwezi Juni 2024. Vivyo hivyo, Kiwango cha faida kwa mikopo ya siku miongoni mwa benki kiliongezeka hadi asilimia 7.9 kutoka asilimia 7.2.

Viwango vya faida kwa Dhamana za serikali za muda mrefu vilionesha mabadiliko sokoni, hususani katika kipindi cha pili cha mwaka wa fedha 2024/25. Mabadiliko sokoni yalitokea baada ya benki kuu husika kubadili utaratibu na mfumo wa upatikanaji wa kuponi (faida) za dhamana za serikali. Aidha, utaratibu ulibadilishwa kutoka mfumo wa kuwa na viwango visivyobadilika kwenda mfumo wenye viwango vinavyobadilika kutegemea hali ya soko.

Mabadiliko hayo yalisababisha kupungua kwa viwango vya faida kwa dhamana za muda mrefu na kuongezeka kwa faida kwa dhamana za muda mfupi na wa kati (Jedwali Na. V). Kwa mujibu wa Benki Kuu, mabadiliko haya yalifanyika ili kuakisi hali halisi ya soko kwa wakati huo.

***Jedwali Na. V: Mabadiliko ya Viwango vya Faida (Coupon Rates): Dhamana za Serikali za muda mrefu.***

| Na. | Maelezo | | Miaka 2 | Miaka 5 | Miaka 10 | Miaka 15 | Miaka 20 | Miaka 25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 | Kabla ya Mabadiliko | Kuponi | 7.60% | 9.18% | 11.44% | 13.50% | 15.49% | 15.95% |
| | | Faida | 11.64% | 12.40% | 13.25% | 15.76% | 15.70% | 15.93% |
| 2.0 | Baada ya Mabadiliko | Kuponi | 12.50% | 13.00% | 14.00% | 14.50% | 15.25% | 15.75% |
| | | Faida | 12.08% | 12.94% | 14.25% | 14.62% | 14.50% | 14.83% |

Viwango vya riba na faida katika benki za biashara, riba za mikopo na faida za amana hazikubadilika kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na mwaka uliopita. Kiwango cha jumla cha riba ya mikopo kilikuwa wastani wa asilimia 15.6, huku kiwango cha mikopo ya mwaka mmoja kikiwa asilimia 15.8. Viwango vya faida kwa amana za jumla na za muda wa mwaka mmoja vilikuwa asilimia 9.7 na asilimia 8.7, mtawalia. Mnamo Januari 2025, Benki Kuu ilibadilisha mfumo wake wa sera ya fedha kutoka kulenga jumla ya fedha kwenye mzunguko hadi kulenga viwango vya faida sokoni. Kufikia Juni 2025, kiwango cha riba cha Benki Kuu (CBR) kwa benki za biashara kilibaki kuwa asilimia 6.0.

Uwepo wa hali stahimilivu ya viwango vya faida na maendeleo ya soko kwa ujumla ni muhimu na husaidia kutoa matarajio chanya kwa wawekezaji na mifuko ya UTT AMIS.

## 4.7 Soko la Kubadilisha Fedha za Kigeni

Hadi tarehe 30 Juni 2025, akiba ya fedha za kigeni nchini ilikuwa zaidi ya Dola za Marekani bilioni 6.0, ambapo Benki Kuu ilikadiria kuwa kiwango hiki kinatosha kwa matumizi ya kulipia huduma na bidhaa kutoka nje ya nchi kwa takribani miezi minne. Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa shilingi 2,631.3, ikilinganishwa na shilingi 2,640.0 mwezi Juni 2024. Kwa kipindi cha mwaka mmoja, thamani ya shilingi iliongezeka kwa asilimia 0.3, ikilinganishwa na hali ilivyokuwa mwaka jana ambapo thamani ilipungua kwa asilimia 12.8 (Jedwali VI).

Kuendelea kufanya vizuri kwa fedha ya Tanzania kumechagizwa na hatua mbalimbali ambazo mamlaka husika zimechukua ili kuendelea kuimarisha thamani ya fedha yetu. Aidha, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuzuia matumizi ya fedha za kigeni kwa manunuzi na malipo ya huduma na bidhaa nchini. Vilevile, mwezi Oktoba 2024, Benki Kuu ilianzisha mpango wa kununua dhahabu kama sehemu ya mkakati wake wa kuongeza kiwango cha akiba ya fedha za kigeni. Pamoja na mambo mengine, hatua hizi zinatarajiwa kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya shilingi ya Tanzania.

***Jedwali Na. VI: Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni Shilingi/USD***

| Mwaka | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Viwango vya Kubadilisha Fedha | 2,300.9 | 2,307.9 | 2,310.4 | 2,315.7 | 2,339.1 | 2,640.0 | 2,631.3 |

Kuimarika kwa thamani ya fedha ya Tanzania dhidi ya fedha za kigeni ni muhimu kwa mifuko ya UTT AMIS na Uchumi kwa ujumla. Hali hii husaidia faida zitokanazo na uwekezaji kuendelea kuwa nzuri na za kuvutia kwa wawekezaji walio ndani na nje ya nchi. Mifuko ya UTT AMIS hutoa faida shidani ingawa huathiriwa na kuleta mabadiliko ya kiwango cha fedha endapo thamani ya shilingi ya Tanzania inapoongezeka au kupungua.

## 4.8 Soko la Mitaji na Dhamana

Kiwango cha uwekezaji na ushiriki wa wawekezaji katika soko la mitaji na dhamana kiliongezeka katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2025 ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), idadi ya wawekezaji iliongezeka kwa asilimia 16.8 mwaka 2024, na kufikia 1,060,509. Ongezeko hili limechagizwa na maendeleo ya soko, elimu na matumizi ya teknolojia katika uwekezaji, hali ambayo imerahisisha na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Miongoni mwa maendeleo ya soko yaliyotekelezwa katika kipindi hicho ni pamoja na mabadiliko ya mfumo wa upatikanaji wa viwango vya faida (coupon rates) na bei za hisa sokoni. Aidha, mabadiliko hayo yameleta mwenendo na hali mpya kwenye viwango vya faida na bei za hisa sokoni.

Katika kipindi cha mwaka mmoja, washirika wengi sokoni wameendelea kutoa kipaumbele zaidi kwenye uwekezaji unaozingatia mazingira, jamii na utawala (ESG) pamoja na maadili ya dini ya kiislamu (Shariah).

### 4.8.1 Soko la Awali

Katika soko la Dhamana za serikali za muda mfupi, kiasi kilichotolewa kilipungua kwa shilingi trilioni 0.1 na kufikia shilingi trilioni 2.6. Vilevile, upande wa mahitaji, kiasi kilichonakiriwa kilipungua kwa shilingi trilioni 1.0 hadi shilingi trilioni 3.3 kutoka shilingi trilioni 4.3. Jumla ya kiasi kilichochukuliwa kilipungua kwa shilingi trilioni 0.7 kutoka shilingi trilioni 2.6 hadi shilingi trilioni 1.9 mwaka 2025.

Kwenye soko la Dhamana za serikali za muda mrefu, Kiwango cha mauzo na ushiriki sokoni kiliongezeka ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Aidha, kwa kipindi hicho kiwango kikubwa cha uwekezaji kilifanyika kwenye dhamana za muda mrefu ikilinganishwa na zile za muda mfupi sokoni.

Jumla ya shilingi trilioni 4.2 zilitolewa kwa mauzo ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.3 mwaka uliopita. Kiasi kilichopokelewa na Benki Kuu kiliongezeka kwa shilingi trilioni 2.0 hadi shilingi trilioni 7.2 ikilinganishwa na shilingi trilioni 5.2 mwaka jana. Kiasi kilichofanikiwa kuchukuliwa kiliongezeka kwa shilingi trilioni 1.0 hadi shilingi trilioni 3.8 kutoka shilingi trilioni 2.8 mwaka 2024.

Katika soko la Hatifungani za kampuni binafsi, soko limenakiri ongezeko la shughuli nyingi kwa upande wa mauzo, washiriki wapya, na mengineyo. Katika kipindi hicho, benki tano za biashara zilitangaza fursa za uwekezaji wenye thamani ya shilingi trilioni 1.2, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali VII.

*Jedwali VII: Orodha ya Hatifungani za Kampuni binafsi zilizoorodheshwa*

| Idadi | Taasisi / Kampuni | Maelezo | Muda | Faida | Tarehe iliyotolewa | Zaidi (-)/chini (+) ya matarajio |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 | Benki ya PBZ | SUKUK Bond | Miaka 7 | 10.5% | 17 Feb 2025 | -12.0% |
| 2.0 | Benki ya CRDB | Samia Infrastructure Bond | Miaka 5 | 12.0% | 10 Feb 2025 | -215.4% |
| 3.0 | Benki ya Azania | Bondi Yangu | Miaka 3 | 12.5% | 17 Jan 2025 | -210.9% |
| 4.0 | Benki ya NBC | Twiga Bond | Miaka 5 | 10.75 | 10 Oct 2024 | -130.0% |
| 5.0 | Benki ya Stanbic | Stanbic Bond | Miaka 5 | 12.5% | 11 Oct 2024 | Haihusiani |

Katika kipindi hadi Juni 2025, soko la Mifuko ya uwekezaji wa pamoja nchini liliendelea kukua na kufanya vizuri ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Kwa kipidi hicho, soko lilionesha ongezeko la wasimamizi, mifuko mipya na idadi ya wawekezaji. Hata hivyo, mifuko mipya iliyoanzishwa, inaashiria ukuaji wa soko na kuimarika kwa utamaduni wa kujiwekea akiba miongoni mwa watanzania na wawekezaji wote kwa ujumla.

### 4.8.2 Soko la Upili

Katika soko la Upili, jumla ya miamala ya Dhamana za serikali iliyofanyika ilikua kwa shilingi trilioni 0.7 na kufikia shilingi trilioni 4.2 ikitoka shilingi trilioni 3.5 mwaka uliopita.

Kwa Hatifungani za kampuni binafsi zilizoorodheshwa, thamani ya miamala ilikuwa shilingi bilioni 9.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3.9 mwaka jana. Aidha, ongezeko la thamani ya miamala ya hatifungani kwa kipindi hicho lilisababishwa na uwepo wa hatifungani mpya na mauzo ya hatifungani zilizokuepo sokoni.

### 4.8.3 Soko la Hisa

Kufikia tarehe 30 Juni 2025, ukubwa wa soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) ulifikia shilingi trilioni 19.6, ikiwa ni ongezeko la shilingi trilioni 2.8 kutoka shilingi trilioni 16.8 iliyonakiriwa tarehe 30 Juni 2024. Wastani wa ushiriki sokoni kwa wawekezaji wa ndani ya nchi ni asilimia 90.6, ikilinganishwa na asilimia 76.2 mwaka 2024.

Fahirisi ya Hisa za kampuni za ndani (TSI), ambayo hufuatilia utendaji wa kampuni zilizoorodheshwa nchini, iliongezeka kwa asilimia 8.4 hadi kufikia 4,852.3. Fahirisi ya kampuni zote sokoni (DSEI) ikijumuisha zile za nje na ndani ya nchi iliongezeka kwa asilimia 16.7 na kufunga mwaka katika kiwango cha 2,353.8. Jumla ya mauzo ya soko katika kipindi hicho yaliongezeka kwa shilingi bilioni 134.9 hadi shilingi bilioni 407.3 kutoka shilingi bilioni 272.4 mwaka uliopita.

Baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa zilitangaza na kulipa gawio kwa wanahisa kama ifuatavyo:TCC: shilingi 850 kwa kila hisa, TPCC: shilingi 600 kwa kila hisa, TBL: shilingi 1,259 kwa kila hisa, NMB: shilingi 428.85 kwa kila hisa, SWISS: shilingi 70.72 kwa kila hisa, VODA: shilingi 20.2 kwa kila hisa, DSE: shilingi 125.5 kwa kila hisa na CRDB: shilingi 65 kwa kila hisa.

### 4.8.4 Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (CIS)

Uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (CIS) uliendelea kufanya vizuri katika mwaka wa fedha ulioishia mwezi Juni 2025. Katika kipindi hicho, idadi ya wasimamizi na mifuko iliongezeka sokoni ikilinganishwa na kipindi kilichopita.

Hadi tarehe 30 mwezi Juni 2025 ukubwa wa mifuko sokoni ulifikia shilingi bilioni 3,272.3 ukilinganishwa na shilingi bilioni 2,273.6 ulionakiriwa mwaka 2024.

#### 4.8.4.1 Mifuko na Huduma za UTT AMIS

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2025, jumla ya thamani ya rasilimali ya mifuko inayosimamiwa (AUM) na UTT AMIS iliongezeka kwa shilingi bilioni 1,030.5, ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 702.8 lililonakiriwa mwaka 2024. Aidha, jumla ya rasilimali ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 2,238.2 hadi shilingi bilioni 3,268.7. Ongezeko hilo la rasilimali, linaashiria kuongezeka kwa imani ya wawekezaji katika fursa za uwekezaji zinazosimamiwa na UTT AMIS.

Live Well ...You Deserve It

Kwa upande wa UTT AMIS, kuingia kwa wasimamizi wapya wa mifuko ya uwekezaji na fursa zingine mpya ni kiashiria chanya cha ukuaji na kuimarika kwa imani katika soko la mitaji na dhamana. Uwepo wa fursa mpya za uwekezaji, na kuongezeka kwa wasimamizi wa mifuko nchini kunasaidia kukuza utamaduni wa kujiwekea akiba, huongeza ukwasi, na kuchochea ushindani wenye afya sokoni.

Kutokana na hayo, hali ya utendaji wa mifuko ya UTT AMIS kwa ujumla ilikuwa imara ikilinganishwa na maeneo mengine linganifu. Faida iliyopatikana na ukwasi uliotolewa kwa wawekezaji kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 ilikuwa ya kuvutia na shindani. Hivyo basi, tunajivunia mafanikio yetu kwa pamoja na kuahidi kuendelea kutoa huduma bora itakayo kidhi matarajio ya wawekezaji tulionao sasa na hata wale watakaowekeza nasi kwa siku zijazo.

## 4.9 Huduma Jumuishi Za Kifedha

Kukua kwa huduma jumuishi za kifedha nchini Tanzania zimechochewa kwa kiasi kikubwa na maendeleo ya kiteknolojia na ubunifu wa huduma na bidhaa. Kwa mujibu wa taarifa ya mwaka ya Ujumuishaji wa matumizi ya huduma na bidhaa za kifedha iliyotolewa na Benki kuu, idadi ya vituo vya upatikanaji wa huduma za kifedha iliongezeka kwa asilimia 9.7 mwaka 2024, kufikia vituo 417, ikiwa ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na asilimia 2.3 ya mwaka 2023. Ukuaji huu ulitokana hasa na kuongezeka kwa idadi ya vituo, Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (CIS), Wasimamizi wa Mifuko, madalali wa soko la Hisa la Dar Es Salaam (LDM), Washauri wa Uwekezaji, na waangalizi wa mifuko.

Kwa upande wa UTT AMIS, hadi tarehe 30 Juni 2025, jumla ya rasilimari zinazosimamiwa na Taasisi ya UTT AMIS ni shilingi trilioni 3.2. Kiasi hiki cha fedha kinatafsiri jumla ya thamani ya uwekezaji uliowekezwa kwenye soko la dhamana na mitaji nchini kwa niaba ya wawekezaji kwa kipindi hicho. Aidha, uwekezaji kwenye mifuko ya UTT AMIS huwekezwa kwenye maeneo kama vile, hatifungani za kampuni binafsi na hisa zilizoorodheshwa, amana za benki, na dhamana za serikali. Mifuko hii huwapa Watanzania fursa ya kuwekeza zaidi ya akaunti za kawaida za akiba.

Taasisi ya UTT AMIS kupitia mifuko yake, tumeweza kuanzisha kampeni mbalimbali, ili kuhamasisha umma kuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba. Taasisi, imeanzisha programu na kampeni mbalimbali

kama vile Kijiwe Mchongo na imehamasisha umma kuwekeza kwa kidijitali. Elimu inayotolewa na mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita yamewezesha jamii kufikia malengo yake na kudumisha zaidi utamaduni wa kuweka akiba na kuwekeza kwenye soko la dhamana na mitaji nchini.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja, UTT AMIS ilifanikisha kufungua akaunti mpya 134,768 kupitia simu za mkononi za wawekezaji, na kufanya uwekezaji (kununua vipande) wenye thamani ya shilingi bilioni 86.6. Hata hivyo, wawekezaji waliuza vipande kwa njia ya simu za mkononi vyenye thamani ya shilingi bilioni 235.2, kiasi ambacho kililipwa kwenye akaunti zao za benki.

Kupitia mchakato wake wa usajili wa wawekezaji, UTT AMIS imehamasisha Watanzania wengi kufungua akaunti za benki, ambazo huhitajika wakati wa kujiunga na ni lazima wakati wa kutoa fedha (kuuza vipande). Zaidi ya hayo, UTT AMIS imewezesha upatikanaji wa mikopo kutoka Taasisi za kifedha kwa kuwaelimisha wawekezaji kuhusu elimu ya fedha na kuruhusu kutumia fedha walizowekeza kama dhamana dhidi ya mkopo.

***Chanzo:*** *Benki kuu ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, UTT AMIS na Soko la Hisa la Dar es Salaam.*

***Bodi na Wafanyakazi wa UTT AMIS tunawatakia wote***
***Msimu wa Sikukuu wenye Furaha na Mafanikio katika mwaka wa 2026.***

***Wekeza Uwezeshwe!***

Jikimu Income Scheme
LIVE WELL ...YOU DESERVE IT

# 9 Jarida la Habari

# Jarida la habari la UTT AMIS [Hadi tarehe 30 Septemba, 2025]

LIVE WELL ...YOU DESERVE IT

## 1.0 Maelezo Mafupi juu ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS

- Hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2025, Kampuni ya uwekezaji ya UTT AMIS inasimamia jumla ya mifuko ya uwekezaji wa pamoja sita (6) ambayo ni : Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Wekeza Maisha,Mfuko wa Watoto, Mfuko wa Jikimu, Mfuko wa Ukwasi na Mfuko wa Hatifungani.
- UTT AMIS inasimamia rasilimali zenye jumla ya thamani ya zaidi ya shilingi Trilioni 3.6
- Mwaka 2017 Kampuni ya UTT AMIS ilianzisha huduma ya usimamizi mali kwa kampuni na watu binafsi iitwayo UTT WEALTH MANAGEMENT yenye uwekezaji wenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 43.1.
- Wawekezaji ni zaidi ya **558,768.**
- Mifuko hii ya uwekezaji wa pamoja hutoa faida shindani na ukwasi ukilinganisha na maeneo mengine linganifu sokoni.

## 2.0 Taarifa za ujumla za Mifuko na huduma iliyoanzishwa na kusimamiwa na kampuni ya UTT AMIS

| NA | JINA LA MFUKO | MAELEZO |
|---|---|---|
| 2.1 | Mfuko wa Umoja | Mfuko ulianzishwa tarehe 16 Mei, 2005. Mfuko huu unalenga zaidi wawekezaji wenye malengo ya muda wa kati na mrefu, jambo ambalo huwawezesha kupata muda wa kutosha kujiwekea akiba na kukuza mtaji wao. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana zilizoorodheshwa. |


**Sifa za mfuko ni:**

- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi [hakuna gharama za kujiunga].
- Wawekezaji ni watu binafsi, vikundi na Taasisi, unaruhusiwa katika mfuko huu.
- Kiwango cha chini cha kujiunga ni vipande 10.
- Gharama ya kujiondoa inayotozwa ni 1% ya thamani halisi ya kipande.
- Mauzo ya vipande hufanyika ndani ya siku 10 za kazi baada ya maombi kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji huo.
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika Taasisi za fedha.

*Jedwali Na. 01; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025*

| Tangu Kuanzishwa [Mei,2005] | Miaka 15 | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15.1% | 16.8% | 15.5% | 16.6% | 12.0% | 11.4% |

*Chati Na. 01; ; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025*



2.2 **Mfuko wa Wekeza Maisha**

Mfuko ulianzishwa tarehe 16 Mei, 2007. Mfuko huu unatoa faida za aina 2 ambazo ni, faida ya kukuza mtaji pamoja na faida ya bima. Katika Mfuko huu, zaidi ya asilimia 99.0 ya rasilimali huwekezwa na kiasi kilichobaki hupelekwa katika huduma za bima. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana.

**Sifa za mfuko;**

- Mfuko unaruhusu mwekezaji mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 55 kujiunga.
- Mfuko una aina mbili za mpango wa kuwekeza: (a) kuwekeza kwa awamu na (b) kuwekeza kwa mkupuo.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo [hakuna gharama za kujiunga].
- Kwa mpango wa kuwekeza kila mwezi, kiwango cha chini ni shilingi 8,340/= (ikiwa mwekezaji ana lengo la kufikia kiasi cha shilingi Milioni Moja kwa miaka 10).
- Faida za bima zinazopatikana ni: - bima ya maisha, bima ya ajali, bima ya ulemavu wa kudumu na gharama za mazishi.
- Mfuko unampa fursa mwekezaji kuwekeza kwa mpangilio maalumu, mathalani anaweza kuchagua kuchangia kwa mwezi, mara mbili kwa mwaka au mara moja kwa mwaka.
- Mfuko unampa fursa mwekezaji kupanga na kuchagua lengo na mpango wa uwekezaji atakaoutekeleza na kuutimiza ndani ya miaka 10.
- Mwekezaji akifariki mrithi au mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji.

***Jedwali Na. 02; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025***

| Tangu Kuanzishwa [Mei,2007] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| 13.9% | 25.5% | 22.3% | 14.6% | 14.3% |

***Chati Na. 02; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025***



## 2.3 Mfuko wa Watoto

Mfuko ulianzishwa tarehe 01 Oktoba 2008. Mfuko una lengo la kuwanufaisha watoto kwa kujiwekea akiba na kutumia uwekezaji wao kukidhi gharama za shule na kupata mtaji kwa maendeleo ya baadae. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana.


**Sifa za Mfuko;**

- Uwekezaji ni kwa ajili ya mtoto mwenye umri chini ya miaka 18.
- Kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi 10,000/= na kiwango cha nyongeza ni kuanzia shilingi 5,000/= na kuendelea.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo. [ hakuna gharama za kujiunga ]
- Mfuko unatoa Mpango wa kukuza mtaji.
- Mzazi au Mlezi ataruhusiwa kuuza au kupunguza sehemu ya uwekezaji wake pindi mtoto atakapofikisha umri wa miaka 12.
- Taasisi, kampuni na vikundi vinaweza kuwawekezea watoto kama sehemu ya huduma kwa jamii

***Jedwali Na. 03; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025***

| Tangu Kuanzishwa [Okt,2008] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| 13.1% | 18.1% | 20.7% | 15.9% | 15.1% |

***Chati Na. 03; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025***



**2.4 Mfuko wa Jikimu**

Mfuko ulianzishwa tarehe 03 Novemba 2008. Lengo la mfuko ni kuwawezesha wawekezaji kupata gawio kutokana na mapato ya ziada katika vipindi tofauti na kukuza mtaji kwa mwekezaji wa muda mrefu. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana.

**Sifa za Mfuko:**

Aina ya mpango wa uwekezaji

- (a) Mpango wa kukuza mtaji ni kuanzia shilingi. 5,000/= (b) Mpango wa kupata gawio kila robo mwaka (Kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi milioni 2) na (c) Mpango wa kupata gawio kwa mwaka (kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi milioni 1).
- Kiwango cha nyongeza ni kuanzia shilingi 5,000/= kwa mpango wa kukuza mtaji na shilingi 15,000/= kwa mpango wa kupata gawio.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo [ hakuna gharama za kujiunga]
- Mfuko unatoza gharama za kujitoa kama ifuatavyo: (a) 2.0% kwa mwekezaji aliedumu ndani ya mfuko kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja. (b) 1.5% kwa mwekezaji aliedumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya mwaka 1 na chini ya miaka 2. (c) 1% kwa uwekezaji uliodumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya miaka 2 na chini ya miaka 3 na, (d) Uwekezaji uliodumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya miaka 3 hakuna gharama za kujitoa.
- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha pindi anapohitaji (ndani ya siku 10 za kazi baada ya maombi ya kuuza vipande kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS).
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika Taasisi za fedha.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji.


***Jedwali Na. 04; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025***

| Tangu Kuanzishwa [Nov, 2008] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| **17.5%** | 15.2% | 18.4% | 15.7% | 14.0% |

***Jedwali Na. 05; Gawio kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025***

| Taarifa | Shilingi Bilioni | Kwa kila kipande, shilingi |
|---|---|---|
| Tangu Kuanzishwa [Nov, 2008] | 18.0 | 197.5 |
| Mwaka Mmoja [Okt 24-Sept 25] | 1.1 | 12.0 |

***Chati Na. 04; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025***



FUND UKWASI
Uhuru kwa mwekezaj

2.5 **Mfuko Wa Ukwasi (Liquid Fund)**

Mfuko ulianzishwa tarehe 01 Machi, 2013. Ni Mfuko wa wazi ambao unatoa fursa kwa wawekezaji wenye lengo la muda mfupi, wa kati na mrefu. Ni mfuko wa wazi ambao rasilimali zake huwekezwa katika maeneo yenye vipato vya kudumu (fixed income instruments).


**Sifa za mfuko:**

- Kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi 100,000/= na kiwango cha nyongeza kisichopungua shilingi 10,000/=.
- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha zake za mauzo ya vipande, (ndani ya siku 3 za kazi baada ya maombi ya kuuza vipande kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS)
- Mfuko hauna gharama yoyote ya kujiunga wala kujitoa.
- Mfuko unaruhusu watu binafsi,vikundi au Taasisi kuwekeza.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo (hakuna gharama za kujiunga).
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika Taasisi za fedha.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili anaruhusiwa kuendeleza uwekezaji.

*Jedwali Na. 06; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025*

| Tangu Kuanzishwa [Machi, 2013] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| 18.5% | 16.0% | 17.3% | 14.0% | 13.2% |

*Chati Na. 05; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025*



**2.6 Mfuko wa Hatifungani (Bond Fund)**

Mfuko ulianzishwa tarehe 16 Septemba, 2019. Ni mfuko wa wazi ambao rasilimali zake huwekezwa katika maeneo yenye vipato vya kudumu (fixed income instruments). Mfuko una lengo la kutoa gawio, kulingana na faida itakayopatikana na kukuza mtaji kwa wawekezaji wa muda mrefu.

**Sifa za mfuko:**

Kuna aina tatu za mpango wa uwekezaji katika Mfuko huu:

- Mpango wa kukuza mtaji
- Mpango wa gawio kila mwezi na
- Mpango wa gawio kila baada ya miezi sita.

Kiwango cha chini cha kuanza kuwekeza.

(a) Shilingi 50,000 kwa mpango wa kukuza mtaji

(b) Shilingi milioni 10 kwa mpango wa gawio kila mwezi na

(c) Shilingi milioni 5 kwa mpango wa gawio kila baada ya miezi sita.

- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha pindi anapohitaji, (ndani ya siku 10 za kazi baada ya kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS).
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika taasisi za fedha.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili anaruhusiwa kuendeleza uwekezaji.


***Jedwali Na. 07; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025***


| Tangu Kuanzishwa [Sept,2019] | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|
| 16.1% | 14.7% | 13.2% | 13.4% |

***Jedwali Na. 08; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025***

| Taarifa | Shilingi Bilioni | Kwa kila kipande, shilingi |
|---|---|---|
| Tangu Kuanzishwa [Sept,2019] | 107.4 | 69.0 |
| Mwaka Mmoja [Okt 24 - Sept 25] | 38.1 | 12.0 |

***Chati Na. 06; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025***



| | | |
|---|---|---|
| 2.7 | **Huduma ya usimamizi mali /<br><br>UTT Wealth Management** | Huduma hii ilianzishwa mnamo mwaka 2017, kwa kuweka kipaumbele malengo ya kifedha ya watu binafsi, familia, vikundi na Taasisi za ndani na nje ya nchi. Huduma hii hutengeneza uwekezaji kulingana na mahitaji na malengo ya mwekezaji.<br><br>**Sifa za huduma hii:**<br>• Kiwango cha chini cha kuweka ni shilingi milioni 100 na kiwango cha nyongeza ni kuanzia shilingi Milioni 10. Uwekezaji unaweza kutumika kama dhamana.<br>• Huduma hii inampa fursa mwekezaji kuwekeza kwenye uwekezaji wa muda mrefu sokoni huku akipata nafasi ya kuongeza au kuuza sehemu ya uwekezaji wake kulingana na hali ya soko.<br>• Katika kufanikisha huduma hii mwekezaji atalipia asilimia 1.0 kwa mwaka kama gharama ya usimamizi wa rasilimali zake.<br>• Uwekezaji katika huduma hii, unatoa fursa kwa wawekezaji kuchagua mpango wa kupata malipo ya faida kila baada ya miezi 6 na mpango wa kukuza mtaji.<br>• Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji<br><br>***Chati Na. 05; Mwenendo wa Rasilimali kwa Huduma ya Usimamizi Mali, tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025***<br> |
| **3.0** | **Elimu kwa Wawekezaji** | |
| 3.1 | **Unawezaje kujiunga na Mifuko ya UTT AMIS?** | Mtanzania mkazi na asiye mkazi, mtu binafsi, Taasisi, vikundi wawekezaji wawili (Jointly) wanaruhusiwa ku wekeza katika Mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS. Jinsi ya kuweka :<br>• Mwekezaji binafsi anaweza kujiunga kwa kubonyeza *150*82# na kujisajili kwenye programu tumizi (UTT AMIS APP) ambayo inaweza kupakuliwa kwenye 'App Store' au 'PlayStore'<br>• Mwekezaji anatakiwa kujaza fomu ya kufungua akaunti kwa ajili ya kukamilisha usajili (KYC FORM).<br>• Kikundi na Taasisi, wawekezaji wawili (Joint) atajaza fomu ya kufungua akaunti ya UTT AMIS pamoja na viambatanisho vinavyotambulika kisheria (Certificate of Registration,Muhtsari wa Kikao, NIDA za Watia saini n.k) na kuvituma kupitia barua-pepe uwekezaji@uttamis.co.tz au kuleta kwenye Ofisi za UTT AMIS zilizo karibu nawe au Tawi lolote la CRDB au Madalali wote walioidhinishwa na Soko la Hisa la Dar es salaam. Kwa wawekezaji walio nje ya nchi, kwa akaunti ya mtu binafsi au watu wawili watajaza fomu ya kufungua akaunti na kisha kuambatanisha kitambulisho cha uraia.<br>• Baada ya kupata akaunti namba ya Mfuko uliouchagua na kukamilisha taratibu zote za usajili (KYC Form) mwekezaji anaweza kuanza na kuendelea kuwekeza kupitia njia za simu kama vile Mixx by Yas, Mpesa, AirtelMoney, Halopesa. T-Pesa, Azam Pesa na Ezypesa au njia za kibenki kupitia CRDB, NMB, NBC, STANBIC na zingine. |

3.2 **Nini maana ya kiwango cha Mfumuko wa bei? Na jinsi gani inamuathiri mwekezaji?**

Kwa tafsiri rahisi, mfumuko wa bei ni alama inayotafsiri mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa kipindi fulani sokoni. Kuongezeka kwa kiwango cha mfumuko wa bei huashiria kupungua kwa thamani ya fedha au kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma sokoni.

Kuna sababu nyingi za kiuchumi zinazopelekea kutokea kwa hali hii, hususani ongezeko la fedha katika mzunguko kusikoendana na kasi ya ukuaji wa uchumi na hivyo matokeo yake kupelekea mfumuko wa bei.

Kiujumla, vigezo vilivyokubalika kupima viwango vya mfumuko wa bei ni pamoja na Bei za bidhaa za Jumla (Wholesale Price Index)], Bei za mahitaji ya kawaida ya walaji (Consumer Price Index), Mabadiliko ya pato la ndani la nchi (GDP) n.k . Vile vile, Bei za mahitaji ya kawaida ya walaji (Consumer Price Index) inapima gharama za bidhaa mbalimbali za msingi zinazotumiwa na kundi la watu ikiwakilisha makundi yote ya jamii kama kigezo cha upimaji wa uchumi katika nchi.

Ni muhimu kutambua kuwa, kazi ya kuangalia hali ya mfumuko wa bei katika nchi hufanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Jambo la msingi la kujifunza ni kuwa, Katika uchumi wenye mfumuko wa bei, unashauriwa kuwekeza mara kwa mara hata kama kiasi cha kuwekeza ni kidogo. Kwa kujenga nidhamu hio, unaweza usione madhara au athari hasi za kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika uwekezaji.

3.3 **Nini maana ya Faida Jumuishi?**

Kwa ufupi, ni faida inayopatikana kutoka katika uwekezaji ambao hugeuzwa mtaji na hivyo kutoa faida kubwa zaidi hapo baadae tofauti na uwekezaji wa muda maalum ambao faida inayopatikana inatokana tu na muda uliokaa ndani ya uwekezaji.

Je utajali ikiwa utapata faida ya asilimia 10 au 12 katika uwekezaji?

Ukweli ni kuwa, ukizingatia hilo utaweza kutengeneza tofauti kubwa katika ukuaji wa faida na mtaji kadiri muda unavyoenda/unavyoongezeka. Faida itokanayo na kompaundi inatokana na faida kuendelea kuongeza mtaji ambao huleta mapato makubwa kila mwaka. Mapato makubwa au faida kubwa au uwekezaji wa muda mrefu inaongeza kiasi cha mtaji kwa uwiano wa kijiometri.

**Matokeo ya Faida jumuishi.**

Kwa kutumia jedwali hapo chini, unaweza kuona matokeo ya nguvu ya kompaundi na faida zake kutokana na uwekezaji uliofanywa mara moja kwa kiasi cha shilingi 50,000/= na 5,000,000/= katika vipindi mbalimbali na kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

**Jedwali Na. 09;**

| Faida | 12% | | 14% | |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka/Kiasi** | **50,000/=** | **5,000,000/=** | **50,000/=** | **5,000,000/=** |
| 1 | 56,000.00 | 5,600,000.00 | 57,000.00 | 5,700,000.00 |
| 3 | 70,246.40 | 7,024,640.00 | 74,077.20 | 7,407,720.00 |
| 5 | 88,117.08 | 8,811,708.42 | 96,270.73 | 9,627,072.91 |
| 10 | 155,292.41 | 15,529,241.04 | 185,361.07 | 18,536,106.57 |
| 20 | 482,314.65 | 48,231,465.47 | 687,174.49 | 68,717,449.36 |

Jedwali namba 10, linaonesha matokeo ya nguvu ya kompaundi kutokana na faida zake kwa uwekezaji uliofanywa mara moja kwa kiasi cha shilingi milioni hamsini (50) na shilingi milioni mia moja (100) katika vipindi mbalimbali na kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

**Jedwali Na. 10;**

| Faida | 12% | | 14% | |
|---|---|---|---|---|
| Mwaka/ Kiasi | 50,000,000/= | 100,000,000/= | 50,000,000/= | 100,000,000/= |
| 1 | 56,000,000.00 | 112,000,000.00 | 57,000,000.00 | 114,000,000.00 |
| 3 | 70,246,400.00 | 140,492,800.00 | 74,077,200.00 | 148,154,400.00 |
| 5 | 88,117,084.16 | 176,234,168.32 | 96,270,729.12 | 192,541,458.24 |
| 10 | 155,292,410.42 | 310,584,820.83 | 185,361,065.71 | 370,722,131.41 |
| 20 | 482,314,654.66 | 964,629,309.33 | 687,174,493.59 | 1,374,348,987.19 |

Nguvu ya kompaundi na faida yake inaoneshwa kwenye majedwali yafuatayo kwa mwekezaji anaewekeza kiasi cha shilingi 50,000/=, 100,000/=, 500,000/=, na shilingi milioni 1 kwa kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

**Jedwali Na. 11;** Uwekezaji wa shilingi 50,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 628,278.40 | 634,125.15 | 640,037.27 |
| 36 | 3 | 2,089,091.05 | 2,153,843.92 | 2,221,139.98 |
| 60 | 5 | 3,871,853.61 | 4,083,483.49 | 4,309,756.26 |
| 120 | 10 | 10,242,248.95 | 11,501,934.47 | 12,953,445.60 |
| 240 | 20 | 37,968,441.80 | 49,462,768.27 | 65,058,300.25 |

**Jedwali Na. 12;** Uwekezaji wa shilingi 100,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 1,256,556.81 | 1,268,250.30 | 1,280,074.54 |
| 36 | 3 | 4,178,182.11 | 4,307,687.84 | 4,442,279.95 |
| 60 | 5 | 7,743,707.22 | 8,166,966.99 | 8,619,512.51 |
| 120 | 10 | 20,484,497.89 | 23,003,868.95 | 25,906,891.21 |
| 240 | 20 | 75,936,883.60 | 98,925,536.54 | 130,116,600.51 |

**Jedwali Na. 13;** Uwekezaji wa shilingi 500,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 6,282,784.05 | 6,341,251.51 | 6,400,372.68 |
| 36 | 3 | 20,890,910.55 | 21,538,439.18 | 22,211,399.75 |
| 60 | 5 | 38,718,536.09 | 40,834,834.93 | 43,097,562.55 |
| 120 | 10 | 102,422,489.45 | 115,019,344.73 | 129,534,456.05 |
| 240 | 20 | 379,684,417.99 | 494,627,682.69 | 650,583,002.53 |

**Jedwali Na. 14;** Uwekezaji wa shilingi 1,000,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 12,565,568.09 | 12,682,503.01 | 12,800,745.36 |
| 36 | 3 | 41,781,821.09 | 43,076,878.36 | 44,422,799.50 |
| 60 | 5 | 77,437,072.17 | 81,669,669.86 | 86,195,125.10 |
| 120 | 10 | 204,844,978.90 | 230,038,689.46 | 259,068,912.10 |
| 240 | 20 | 759,368,835.99 | 989,255,365.39 | 1,301,166,005.06 |

Kutokana na jedwali hapo juu, utagundua kuwa sio busara kupoteza muda na pesa. Inabidi utambue kuwa, MUDA ni kigezo muhimu katika kufanya maajabu ya kompaundi.

**Jambo la msingi la kujifunza:**

(1) Wakati wote, tumia fursa zilizopo katika uwekezaji kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni; usalama, ukwasi pamoja na kiwango cha faida.

(2) Endelea kuwekeza kwa muda mrefu ili unufaike na maajabu ya kompaundi.

Taasisi ya UTT AMIS inatarajia kuanza kupokea na kujibu malalamiko, maswali au maoni ya wawekezaji kidijitali (Digital Portal). Aidha, kwa sasa mwekezaji anaweza kuwasiliana nasi kwa kutuma ujumbe kwenda namba ya **WhatsApp +255 753 999 113** na kisha kupata majibu ya maswali au maelezo anayoyahitaji.

Vilevile, kupitia ukurasa wetu wa tovuti **www.uttamis.co.tz**, mwekezaji anaweza kutupata na kuhudumiwa kupitia jukwaa la **Chatbot**.

## 4.0 Mawasiliano

Kwa maelezo zaidi kuhusu Mifuko yetu, tafadhali wasiliana nasi kwa anuani zifuatayo:

**Ofisi ya UTT DAR ES SALAAM**
Ofisi za UTT AMIS Dar es Salaam
Afisa Mtendaji Mkuu,
UTT AMIS Plc,
Ghorofa ya Pili (2), Jengo la Sukari, Mtaa wa Sokoine Drive na Ohio,
S.L.P 14825, Dar es Salaam
Simu Namba: +255 (0) 22 2128460
Namba za Bure: 0800112020
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz
Tovuti: www.uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS MBEYA**
Ghorofa ya Pili, Jengo la NHIF, Mbeya
S.L.P 1210, Mbeya,
Simu Namba: +255 (0) 25 2500371
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS MWANZA**
Mezzanine, Jengo la NSSF Commercial Complex
S.L.P 640, Mwanza,
Simu Namba: +255 (0) 28 2505072
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS DODOMA**
Ghorofa ya Sita, Jengo la PSSSF,
Mtaa wa Makole,
S.L.P 1310, Dodoma
Simu Namba: +255 (0) 26 2323861
Nukushi: +255 26 2323862
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS ARUSHA**
Ghorofa ya Nne, Jengo la Ngorongoro Conservation,
S.L.P 2490, Arusha,
Simu Namba: +255 (0) 27 2970625
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS ZANZIBAR**
Ghorofa ya Tatu, Jengo la Sheikh Thabit Kombo- Michenzani
S.L.P 2190, Zanzibar
Simu Namba: +255 (0) 24 2941274
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya MOROGORO**
Ghorofa ya Tatu, Jengo la Shirika la Nyumba
Barabara ya Dar es Salaam
Simu Namba: 0800 112020
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya KAHAMA**
Jengo la NSSF Mafao,
Simu Namba: 0800 112020
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya DAR ES SALAAM**
Ghorofa ya chini
Jengo la PSSSF Complex
Barabara ya Sam Nujoma
S.L.P 14825
Dar es Salaam
Simu Namba: Toll free 0800112020
Barua Pepe. uwekezaji@uttamis.co.tz

Jikimu Income Scheme

LIVE WELL ...YOU DESERVE IT

# Ishi vizuri... Unastahili

## Mifuko Mingine ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS